Tawba

Tawba

Sayyid Abdul Husayn Dastghaib Shirazi

Kimetafsiriwa na
Amiraly M. H. Datoo

Al-Islam.org

Author(s):

Sayyid Abdul Husayn Dastghaib Shirazi [1]

Kitabu hiki kinazungumzia Tawba katika Islam, fadhila zake na faida zake katika maisha ya mwanadamu. Pia kinajadili jinsi ya kutubu tulivyofundishwa na Quran, Mtume Muhammad (SAW) na Aimma.

Get PDF [2] Get EPUB [3] Get MOBI [4]

Translator(s):

Amiraly M. H. Datoo [5]

Topic Tags:

Tawbah [6]

Kutoka Kalamu Ya Mtayarishaji

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, mwenye kurehemu.

Sifa zote ni za Allah swt Mola wa dunia zote na salaam zimfikie Mtume wake Muhammad s.a.w.w. pamoja na ahali yake Tahirifu a.s.na Sahaba Muttaqiina.

Vijana wetu katika zama hizi wapo wanasikitikia na kujutia juu ya yale waliyoyatenda, lakini kwa kuwa hawana mategemeo, basi wapo wanaendelea na matendo yao maovu.Wanafikiri kuwa sasa wameshatenda madhambi na hawajui kama watasamehewa au la, na hivyo utawaona wakiupoteza ujana wao katika maasi mbele ya Allah swt. Hivyo nimeonelea afadhali niketi na kukitayarisha kitabu hiki cha *TAWBA* pamoja na kutarjumu mengi ya makala ya Shahid Mihrab Muallim Akhlaq Ayatullah Shahid-i-Dastaghib Shirazi juu ya *TAWBA* katika lugha ya Kiswahili ili kuwanufaisha vijana na wazee.

Iwapo kazi hii ndogo itaweza kuiathiri roho ya mtu au nafsi yake, ingawaje mmoja tu, basi itakuwa ni furaha yangu.Ingawaje matamanio ya mwanadamu ni mengi mno kupita kiasi, lakini umri wake upo unamnyima nafasi hiyo. Kila usiku na mchana kunapozunguka kunampunguzia umri wa mwanadamu huyo, wala mwanadamu kutoka dunia hii na kama vile tujuavyo kuwa mauti itatujia siku moja na kutuchukua kutoka humu duniani. Iwapo mwanadamu amekwisha tenda madhambi katika maisha yake huku duniani, basi asikate tamm bali inmbidi ajitokeze mbele ya Allah swt kwa taadhima na heshima kwa kuomba *TAWBA* na MSAMAHA, na kwa hakika Allah swt lazima atatusamehe. Allah swt yupo kila

wakati akisema: 'Ewe Mja wangu! na kamwe hujatuita;Ewe mwovu, muasi au jina lingine lolote lililo ovu, Ilhali unazijua aibu zetu, lakini kazificha. Sisi tunapojua aibu za mtu miongoni mwetu, basi huwa tunamwona kwa mtazamo wa dharau, lakini Allah swt amezificha aibu zote.

Mtu anapokuwa akilaumiwa na dhamira yake, akili yake na nafsi yake kumfanya au kumshurutisha afanye*TAWBA*, basi asiwe na wasiwasi, ila ajielekeze katika kufanya *TAWBA* YA ALLAH swt na hivyo atoe ahadi yake thabiti ya kutotenda madhambi tena. Hapo ndipo Allah swt anaposema kuwa kilio cha mwenye madhambi ni afadhali kuliko tasbihi za Malaika.

Kwa mujibu wa Ahadith na riwaya mbalimbali, madhambi ya mfanya *TAWBA* hudondoka kama vile yanavyodondoka majani katika mti au mfano wa mtoto mchanga anapozaliwa huwa hana madhambi. Hivyo inambidi mtu asiendelee kufanya madhambi baada ya kufanya *TAWBA* wala tusisite kuomba *TAWBA* kwa ajili ya madhambi tuliyokwisha tenda hapo kabla.

Ayatullah Dastaghib Shirazi, alikuwa ni shakhsiyyah mashuhuri sana huko katika Jamhuri ya Kiislamu Iran. Nchi hiyo haitaweza kamwe kusahau mchango wake katika nyanja nyingi za : elimu, dini n.k. Alipokuwa akitoa hotuba zake, basi nywele za wasikilizaji ziliweza kusimama na kujawa kwa hofu ya Allah swt, miili yao ilikuwa ikitetemeka. Maneno yake yalikuwa ni kama jawhari zenye thamani kubwa mno.

Laana ziwe juu ya maadui wa Islam ambao hawakupendezewa kuishi kwake humu duniani na maluuni mmoja asiye na huruma alimwua akiwa katika Mihrabu kwa mlipuko wa bomu. Shahidi Mahrabu (alijulikana tangia hapo) alipokufa shahidi kama Babu yake al-Imam Ali a.s. ambaye pia aliuawa kwa upanga wa ibn Muljim akiwa katika
Mihrab.Tunamwomba Allah swt amweke mahala pema na kumrehemu, pamoja na Mitume a.s. na ma-Imamu a.s.

Katika utafiti wangu nilioufanya, nimejaribu kwa uwezo wangu kuongezea pale nilipohisi palihitajika na vile vile hapo mwishoni nimeongezea aya za Quran zizungumziazo *TAWBA*, pamoja na Hotuba ya Imam Ali (a.s.) kutoka Nahjul Balagha na Doa Na. 31 kutoka Sahifa-i-Sajjadiyyah juu ya *TAWBA*.

Ni matumaini yangu kuwa kazi hii ndogo itatusaidia sote na tuombe kwa Allah swt aikubalie na kutujaalia tawfiqi ya kutenda matendo mema na tukifariki tuwe miongoni mwa wale waliokwisha fanya *TAWBA*.

Amiraly M.H.Datoo,
23 Desemba,1990 A.D
5 Jamadiul Aakhar 1411 A.H
P.O.Box 838,
Bukoba - Tanzania.

1. Tawba

Allah swt katika **sura Tahrim** Aya ya 8 anatuambia:

"Enyi mlioamini! tubuni kwa Mwenyezi Mungu TAWBA iliyo ya kweli....." (***66 : 8***)

Kwa watu wenye kuona na kufikiri, haikufichika kwao kuwa *TAWBA* ni fungu mojawapo la ukarimu na rehema za Allah swt na kwamba *TAWBA* ni mlango mmojawapo mzuri kabisa ambao Allah swt ametufungulia ukawa wazi daima kwa ajili ya sisi waja wake. Iwapo mlango huu wa *TAWBA* ungalikuwa umefungwa, basi hakuna mtu ambaye angeweza kuokoka na kufanikiwa mbele ya Allah swt, kwani maisha na matendo yake mwanadamu yamejaa makosa, madhambi na maasi.

Ndiyo hivyo ilivyo kuwa kila mtu amekuwa akijitumbukiza katika shughuli fulani fulani ambapo ni Allah tu ndiye aliyekuwa akimhifadhi na kumsitiria hayo maovu yake. Kwa kifupi ni kwamba mwanadamu anaweza kujizuia asitende madhambi, lakini hakuna mtu anayeweza kudai kuwa yeye hakutenda madhambi tangu alipopata akili, isipokuwa Mitume a.s. na ma–Imamu a.s. ambao hatuna shaka na utoharifu wao.

Ni kwa sababu hiyo Allah ametuwekea dawa ya kutuponyeshea magonjwa yetu na maradhi ya kiroho na ni njia ya kuyasafisha matendo yetu maovu, ili kwa baraka za *TAWBA*, madhambi ya mwanadamu yaishe na aweze kujipatia uokovu wa milele.

Amebahatika mtu ambaye ameweza kuuthamini huu mlango wa rehema na kuweza kufaidika nao akawa mpenzi wa allah swt na ameweza kuwa mja mwenye kushukuru neema zake. Lakini hakubahatika yule ambaye hakuweza kufaidika kwa mlango huo ambapo milango na njia zote za *TAWBA* zimekuwapo wazi mbele yake!

Siku ya Kiyama wakati wa kutoa hisabu, mtu atakapokuwa akijitafutia visingizio na sababu katika kujibu maswali atasema: Ewe Mwenyezi Mungu! Mimi nilikuwa mjinga na wala sikuwa na habari, matamanio na ghadhabu zangu zilinifunga kwa minyororo na wala sikuweza kamwe kumudu msimamo wangu dhidi ya wasiwasi na upotofu wa Sheitani." Hapo atajibiwa pamoja na masingizio na sababu zake "Je, sikukuwekea wazi njia zote za *TAWBA*? Ulielezwa kazi zote zilizo ngumu, na je alitokea yoyote mwenye kuzidi uwezo wako? Je, masharti ya *TAWBA* yalikuwa hayakushughulishi wewe?"

Hapa ninaonelea vyema kuelezea machache juu ya *TAWBA*.

2. Uhakika Wa Tawba

Ipo Hadithi ya Mtume (S.A.W.W.) isemayo:
"Majuto na masikitiko baada ya kutenda dhambi ndiyo *TAWBA*."

Imam Muhammad Al-Baqur (a.s.) amesema:
"Kule kusikitika kwa mtu baada ya kutenda matendo,inatosha kwa kufanya *TAWBA* .....(*Usuli Kafi*)

Al-Imam Jaafer as-Sadique (a.s.) amesema:
"Hapana mtu ambaye asiyesamehewa na Allah swt baada ya kusikitika na kujuta kwa yale aliyoyatenda, na anapoomba msamaha na kutubu, basi hapo madhambi yake yote kwa pamoja husamehewa....."

Kwa sababu hiyo uhakika wa *TAWBA* ni kusikitika, kujuta na vile vile kujihisi mtu mwenye aibu kwa madhambi tuliyuoyatenda. Inambidi mtu aamini kuwa Allah swt atachukizwa kwa kosa langu hili kama vile mja anapofanya jambo kinyume na matakwa ya mmiliki wake huku akionwa na bwana wake, akiwa katika hali ya kumsahau Tajiri wake. Kwa kuwa kila mtu anaelewa na kuamini pia kuwa chochote kile akitendacho Allah swt anamwona, basi hapo kwa hakika atakuwa na majuto na masikitiko, na vile vile atakuwa amepatwa na aibu sana kama vile mfanyabiashara mmoja apatanapo na mtu na akampatia vyote alivyokuwa navyo na huku amebakia na deni adaiwalo, basi atasikitika mno kwa mapatano kama hayo. Hususan atasikitika zaidi pale iwapo atakuwa alishakanwa na kuzuiliwa na rafiki mpenzi. Mfano wake ni sawa na mgonjwa ambaye amekatazwa na daktari asile vitu fulani kwani vitamletea madhara mwilini mwake,naye kwa kupuuzia mashauri hayo, akavila, na hatimaye akaugua na kutaabika zaidi. Basi katika hali hiyo hakuna kitu kingine isipokuwa ni masikitiko na majuto matupu.

3. Majuto Na Masikitiko

Sababu Ya Kuepukana Na Madhambi

Kila itakavyokuwa zaidi imani ya mtu na yakini yake juu ya Allah na Kiyama; Mtume s.a.w.w. na ma - Imam a.s. ndivyo vivyo hivyo itakavyokuwa masikitiko yake kwa madhambi yake, na daima atakuwa akisononeka moyoni mwake kwa kujionea aibu. Kwa hivyo pamoja na majuto, masikitiko na aibu, inambidi mtu afikie uamuzi madhubuti katika kuepukana na madhambi kwani asipojizatiti katika kuepukana na madhambi, basi itamaanisha wazi wazi kuwa yeye hanayo majuto wala masikitiko au aibu kwa madhambi atendayo.

Imam Ali a.s. amesema: "Haiyumkini kwa mtu kusikitika na kujuta huku bado akiendelea kutenda

madhambi." Baada ya kusikitika na kujuta kwa madhambi, inambidi mtu atekeleze malipo ya madhambi hayo aliyokuwa akiyatenda. Kama zilikuwa ni haki za Allah swt kama vile sala, saumu, zaka, Hajj n.k. basi baada ya kutubu inamlazimu alipe vyote hivyo.

Iwapo ni *haqqun–naas* (haki za watu) kama vile amechukua mali ya mtu bila ya ruhusa yake, basi airejeshe hiyo mali haraka sana, na iwapo mwenye mali hiyo amefariki, basi awafikishie warithi wake na iwapo hawafahamu warithi wake, basi atoe sadaka kwa niaba ya mwenye mali. Iwapo alikuwa amemvunjia heshima ya mtu, basi amwombe msamaha yule aliyemvunjia heshima ya mtu, basi na afanye kila jitihada ya kumridhisha. Iwapo ni haki ya kisasi au fidia basi inambidi ajipeleke mbele ya mwenye kisasi au fidia ili itekelezwe au asamehewe. Iwapo ni haki ya adhabu iliyopitishwa, kama vile kumzulia mtu jambo asilolitenda, basi ajipeleke mbele ya huyo mtu ili hiyo hukumu itekelezwe au aweze kusamehewa.

Lakini, iwapo yeye amejitwisha madhambi ambayo hukumu zake zimeshatolewa na Allah swt, kwa mfano wa zinaa, basi haimlazimu mtu kujipeleka mbele ya hakimu wa Kiislamu na kuungama ili atimiziwe adhabu inayomstahiki. Kinachombidi yeye katika hali kama hiyo ni kuacha kutenda madhambi hayo, awe anajuta na kusikitika kwa msimamo imara aombe msamaha kwa Allah swt.Ama kwa madhambi yaliyo Makuu (ghunahi kabirah) na adhabu zao hazikuwekwa waziwazi kama vile kuimba na kusikia muziki, basi kwa mujibu wa Aya za Qurani imedhihirika kuwa mtu huyo awe akisikitika na kujuta na hapo aombe maghfirah, yaani aombe kwa Allah amsamehe madhambi yake na kumbariki.

4. Toba Kamilifu

Mtu mmoja alitamka 'Astaghfirullah' mbele ya Imam Ali a.s. Hapo Imam alimwambia: "Ole wako! Je wajua kuwa istighfar ni nini? (Kwani huyo mtu alikuwa akitubia mdomoni tu, wakati moyoni mwake alikuwa hana hisia za kutubu) Istighfar inayo daraja la juu kabisa na ni mojawapo ya mambo bora kabisa mbele ya Allah. Ama katika maana ya Istighfar, ni lazima kuwepo kwa mambo kwa mambo sita katika utekelezaji wake, ndipo itakapokuwa Istighfar kamili:

1. Kujutia na kusikitikia matendo tuliyokwisha tenda.
2. Tuazimie kwa nia moja kutotenda madhambi tena maishani mwetu
na vile vile kuwa tutajiepusha nayo kwa uwezo wetu wote.
3. Kutimiza haki za watu ili tutakapokufa tuwe tumekufa bila ya haki
ya mtu mbele ya Mola wetu (Tusiwe na mzigo wa mtu).
4. Tuzilipe amali zote tulizoziacha na ambazo tulifaradhiwa.
5. Kuugeukia mwili wetu, kusikitika na kujuta katika hali ya *TAWBA*,
hadi nyama yote ilikuwa kwa sababu ya kula vilivyo haramu ikauke

kiasi kwamba ngozi igusane na mifupa. Baada ya *TAWBA*, nyama inaweza kukua kwa mara nyingine tena.
6. Tuuonjeshe mwili wetu taabu na shida za ibada kama vile tulivyokuwa tukiufurahisha wakati wa kutenda madhambi tukiwa katika starehe mbali mbali.

Basi utakapokuwa umejitahidi na umetekeleza hayo mambo sita, ndipo useme '*astaghfirullah*'

5. Fadhila Za Tawba Na Ufaradhi Wake

Maulamaa wote wanaungana pamoja kwa kusema kuwa ni faradhi kufanya *TAWBA* kwa kila dhambi liwapo dogo au kubwa na hivyo ndivyo ilivyo uamuzi wa akili zetu. Allamah Muhaqqiq Tusi (A.R.) katika Tajrid Kalaam na pia katika kusherehesha hivyo. Allamah Hilli (A.R.) wanasema: "*TAWBA* itakuwa ni sababu ya kumwepusha mtu na madhara ya aina yoyote ile na udharura wa kujiepusha na madhara kwa mujibu wa akili yetu ni wajibu. Kwa hivyo, kiakili kutubu ni fardhi!"

Allah swt anatuambia katika ***sura Nuur Aya 31***:-

"Na Tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Muumin ili mpate kufaulu....." (***24:31***)

Na katika ***sura Tahrim***, Aya ya 8 anatuambia:

"Enyi mlioamini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu Toba iliyo ya kweli; huenda Mola wenu akakufuteini maovu yenu....." (***66:8***)

6. Je' Tawbatan – Nasuha' Ni Ipi?

Katika kuisherehesha al-Kafi, Allamah Majlisi (A.R.) anawanakili mufassirina:

1.Kutubu kwa ajili ya furaha ya Allah swt kwa kujitakasa kuwa khalisi, yaani kutofanya *TAWBA* kwa kuwa na khofu ya Jahannam (motoni) au kwa tamaa ya Janati (peponi). Badala yake kuhuzunika na kusikitika kwa matendo tuliyokwisha tenda na vile vile tujiulize '*Je, kwa nini nimefanya hivyo?*' Muhaqqiq Tusi (A.R.) katika Tajiri al-Kalaam anasema kuwa iwapo mtu atajuta na kujiepusha na madhambi kwa khofu ya Jahannam, basi hiyo haitakuwa *TAWBA*!

2.Tufanye *TAWBA* kiasi kwamba wengine watuonapo wapate fundisho, yaani tujitakasishe kwa *TAWBA* hadi mtu mwingine mwenye madhambi atuonapo, naye ashawishike kufanya *TAWBA* au tuwe ni watu wa kutoa nasiha kwa wengineo na vile vile mara kwa mara tusijumuike pamoja na kundi la wenye madhambi duniani na akhera.

3. *Nasiha–khayyat* yaani mtu aionaye dini yake inachanika basi aitu mie *TAWBA* kama sindano ya kushonea machaniko hayo. Wafanyao *TAWBA* pia wamekuwa wakisemwa ni watu walio miongoni mwa Awliya– i–Allah swt.

4. Kila mwenye kufanya *TAWBA*, lazima awe na sifa za Nasuha yaani mtu ajisihi mwenyewe kwa nia khalisi na kwa ukamilifu na hivyo azimalize athari zote za madhambi yake na awe ni mwenye ridhaa na kujipatia nuru ya imani na awe mwenye kutenda matendo mema daima badala ya kutenda maovu hata yawe madogo kiasi gani.

Mwanachuoni mmoja mkongwe aeleza kuwa haitoshi kuufuta moshi mweusi uliotanda moyoni mwetu, bali inatubidi tuusugue, kama vile mtu anavyosugua chuma kwa ajili ya kutoa kutu iliyo juu yake. Hivi ndivyo tunavyopaswa kuangamiza mabaki ya maovu na kuanza kung'ara kwa nuru moyoni mwetu, kwani madhambi tuliyokwisha tenda yametia kiza nzito juu ya nyoyo zetu. Kwa hivyo inatubidi tujitakase kwa njia ya utiifu na ibada.

Kila tutakavyokuwa tukiongeza ibada zetu ndivyo moyo wetu utakuwa ukiingiwa na nuru. Kila mfanya *TAWBA* inambidi aweke madhambi yake mbele yake wakati wa kufanya *TAWBA* ili awe akitubu moja baada ya jingine bila ya kubakiza lolote kati ya maovu yetu tuliyoyatenda hapo awali.

Mfano, iwapo tulikuwa tukipendelea mno kutembelea na kusikiliza muziki na majumba yake, basi inatubidi tusikilize na kuisoma Quran, Hadithi na mawaidha mbalimbali ya dini.(Wakati wa kusoma Quran tufuate sharti la utoharifu). Iwapo tulibakia msikitini katika hali ya janaba basi inatubidi tufanye I'itikafu msikitini.Iwapo tulikuwa tukivitizama vitu ambavyo vimeharamishwa na Allah, basi sasa inatubidi tuvitazame vitu vyote vyema vyenye kuwa na malipo ya thawabu za ibada.Mfano kusoma Quran Tukufu, kuzitazama nyuso za wazazi wetu, kuwatazama wazee na watu walio wema na Masharifu na vile vile tujifunze kwa kuzitazama neema za Allah.

Baada ya kufanya *TAWBA* na baada ya kurejesha haki za watu, sasa tutoe sadaka kwa kiasi kikubwa kutokea mali yetu.Iwapo tulimsengenya mtu yeyote, basi baada ya kutubu, tumsifu huyo mtu kwa wingi kwani tulimsengenya na itatubidi tubainishe matendo yake yaliyo mema.Kwa kifupi, baada ya kufanya *TAWBA*,itatubidi tutende matendo yetu dhidi ya madhambi.Hivyo tuzidishe matendo yetu mema na tuongezee ibada zetu bila ya kujali upinzani utokao katika nafsi zetu kama vile daktari anavyomtibu

mgonjwa ndani ya mwili wake na wala hapendi apasuliwe.Lakini daktari atafanya kinyume na kile atakacho mgonjwa kwa ajili ya faida yake.

7. Fadhila Za Tawba

(a) Mwenye kufanya TAWBA ni mpenzi wa Allah swt.

Allah swt anasema katika **Sura al-Baqarah**, Aya 222:-

"Hakika Allah huwapenda wanaotubu……." (***2:222***)

Al-Imam as-Sadique (a.s.) anasema:

"Allah hufurahia mno toba zifanywazo na Muumin kama vile sisi tunavyofurahi mno wakati tunapomwona rafiki yetu mpenzi aliyekuwa amepotea."(*al-Kafi*)

(b) Maovu kubadilishwa kuwa mema

Kwa kufanya *TAWBA*, kiza cha maovu kitatoka mioyoni na nafasi yake itachukuliwa na nuru. Maovu yetu yatafanywa kuwa mema.

Allah swt anatuambia katika **Sura Furqaan**, aya 68-70:-

"Na wale wasiomuomba Mungu mwingine pamoja na Allah, wala hawaui nafsi aliyoiharamisha Mwenyezi Mungu (***kufanya hivyo***) ***isipokuwa kwa haki*** (***kufanya hivyo***)***, wala hawazini; na atakayefanya hayo atapata madhara yake.Na atazidishiwa adhabu siku ya Kiyama na atakaa humo kwa kufedheheka milele.***

Ila yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri; basi hao (***waliotubu***) ***ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema; na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu."*** (***25:68-70***)

(c) Malaika huwaombea Dua na kuwasifu

Allah swt anatuambia katika sura Muumin, Aya ya 7-9:-

"Wale wanaokikaribia kiti cha Enzi (***cha Mwenyezi Mungu***) ***na wale wanaokizunguka, wanamtukuza Mola wao na kumsifu na wanamuamini na wanwaombea samahani walioamini,*** (***wanasema***)***: "Mola wetu! umekienea kila kitu kwa rehema na elimu*** (***unakijua kila kitu***)***. Basi***

wasamehe waliotubu na wakaifuata njia yako na waepushe na adhabu ya Jahannamu."

"Mola wetu! Waingize katika mabustani ya milele uliyowaahidi. Na uwape haya pia waliofanya mema miongoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao; bila shaka wewe ndiye mweye nguvu, mwenye hekima."

"Na waepushe na maovu, kwani umuepushaye na maovu, kwani siku hiyo, hakika umemrehemu; na huko ndiko kufuzu kukubwa." (***40:7–9***)

(d) Mwenye kutubu ni watu wa Peponi

Allah swt anatuambia katika **sura Ali-Imraan**, aya 135–136:

"Na ambao wanapofanya matendo ya aibu au kudhulumu nafsi zao, hukumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kwa dhambi zao. Na ni nani anayeghufuria dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? Na hawaendelei (***kwa makusudi***) ***yale waliyoyafanya, hali wanajua.***

Hao ndio malipo yao yatakuwa msamaha kwa mola wao na Bustani (***pepo***) ***zinazopita mito mbele yake ambamo watakaa milele. Na ni wema ulioje ujira wa watendao*** (***mema***)***."*** (***3:135–136***)

(e) TAWBA inarefusha maisha

Allah swt anatuelezea katika **sura al-Hud**, Aya ya 3:

"Na ili muombe msamaha kwa Mola wenu; kisha mtubie kwake, atakustarehesheni kwa starehe nzuri mpaka muda maalum. Na atampa kila mwenye fadhila, fadhila zake." (***11:3***)

Imam Jaafer as-Sadique (a.s.) amesema:
"Umri wa baadhi ya watu hupungua kwa sababu ya madhambi yao na wao hufa haraka, na baadhi ya hufariki katika wakati waliopangiwa. Yaani kwa ufupi ni kwamba,madhambi hupunguza umri wa watu wakati ambapo *TAWBA* huongezea umri wake."

(f) TAWBA ni sababu ya kukubaliwa kwa Duaa

Suala hili tutalizungumzia kwa undani zaidi hapo mbele na vile *TAWBA* inavyowezesha kukubaliwa kwa Duaa .

(g) TAWBA ni ujumbe mwema kutoka Allah swt

Allah swt anatuambia katika sura Shuraa, Aya 25:

"Naye ndiye anayepokea TAWBA za watu wake, na anasamehe makosa, na anayajua yote

mnayotenda." **(*26:25*)**

Imam Jaafer as- Sadique (a.s.) amesema:
"Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume Daudi (a.s.):"Ewe Daudi! Wabashirie habari njema watendao madhambi na waja wema uwapatie nuru ya matumaini! Hapo Mtume Daudi (a.s.) aliuliza:Ewe Mwenyezi Mungu! Je, niwabashirie vipi hao wenye madhambi na kuwapa matumaini hao wema?"

Alijibiwa:"Watendao madhambi waambie kuwa mimi nitazikubali *TAWBA* zao.Na hao watu walio wema waambie wawe na matumaini ya malipo yao kutoka kwangu kuliko kujionyesha na kufanya kiburi kwani kwa kufanya hivyo wao watakuwa wamejipotezea urira wao kwangu.Mimi nitachukua hisabu ya kila kitu kiwe kidogo au kikubwa."

(h) TAWBA huangamiza madhambi yote kwa pamoja

Allah swt anasema katika **Sura Zumar** Aya 53-54:

"Sema* (*Ewe Mtume wetu Muhammad!*)*: "Enyi waja wangu! mliojidhulumu nafsi zenu, msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote; hakika yeye ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu."

***"Na rejeeni kwa Mola wenu na mnyenyekee kwake kabla ya kukujieni adhabu, kisha hamtanusuriwa."* (*39:53-54*)**

Katika Aya hii kuna msisitizo mkubwa juu ya kufanya *TAWBA*. Imam ar-Ridha (a.s.) amemsikia sahaba wake kuwa Mwenyezi Mungu anamlaani yule mtu ambaye amepigana na Ali a.s. Basi hapo Imam a.s. alimjibu: "Ila aliyetubu na amekuwa mwema." Akaendelea: "Dhambi iliyo kubwa kabisa kuliko hata kumwua Imam Ali (a.s.) ni kule kumkhilafu bila kutubu." (*Wasail Shia* Vol. 11, page:265, mlango wa *TAWBA* ya madhambi makuu).

Kwa mujibu wa riwaya hiyo tuliyoisoma, inatuelezea wazi kuwa madhambi makubwa pia yanaweza kusamehewa iwapo tutafanya *TAWBA*.

(i) TAWBA iliyoombwa haitobatilika iwapo itavunjwa

Iwapo tuliomba *TAWBA* na tukarejea kutenda dhambi kwa mara ya pili, basi ile *TAWBA* yetu tuliyokuwa tumetangulia kuiomba, haitavunjika au kubatilika, bali inatubidi turejee kuomba *TAWBA* yetu kwa upya. Tujue kuwa kila tutakavyokuwa tukiomba *TAWBA* basi ndivyo vivyo hivyo madhambi yetu yatakuwa yakifutwa.

Muhammad ibn Muslim anaripoti riwaya ambamo Imam Muhammad al-Baquir (a.s.) amesema:"Ewe Muhammad ibn Muslim!Muumin atakapoomba *TAWBA* kwa ajili ya madhambi yake, basi atasamehewa na Allah swt kwani anawapenda waja wake zaidi."Hapo mimi nilimwuliza Imam (a.s.):"Iwapo mtu atatubu

na kurejea dhambi na tena akaomba *TAWBA*."

Imam (a.s.) alimjubu: "Ewe Muhammad ibn Muslim! Wewe waelewa vyema kuwa asikitikapo na kujutia matendo yake maovu na akaomba *TAWBA*, je itawezekanaje kwa Allah kutoikubalia hiyo *TAWBA*?

Niliuliza."Je, iwapo atakuwa akiendelea vivyo hivyo kwa mara nyingi?"

Alijibu Imam (a.s.):"Hivyo pia *TAWBA* yake itakubaliwa na madhambi yake yatasamehewa kwani Allah swt ni mrehemavu mno na mkubalia wa *TAWBA*.Kwa hivyo inambidi Muumin awe na matumani ya kusamehewa madhambi yake."

Abu Basir anasema: "Mimi nilimuuliza Imam Jaafer as-Sadique (a.s.), 'Je, nini maana halisi ya '*Tawba*tan-Nasuha' ambayo Allah swt anatuamrisha?"Imam (a.s.) alijibu:"*TAWBA* ambayo baada yake hakutarudiwa tena kutendwa kwa madhambi."

Hapo nilimuuliza:"Je, kuna mtu yeyote miongoni mwetu ambaye harudii kutenda madhambi kwa mara ya pili au zaidi?"

Imam (a.s.) alinijibu: "Ewe Abu Basir! Mwenyezi Mungu humpenda mno yule mtu aliyepotoka mno na akaja kufanya *TAWBA*."

Vile vile ipo riwaya nyingineyo isemayo:"Ni jambo bora kabisa la kufanya *TAWBA* na kufanya juhudi za kuomba msamaha wa Allah swt kila baada ya kutenda dhambi."

(j) Milango ya TAWBA ipo wazi hadi pumzi ya mwisho

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) amenukuliwa riwaya isemayo:

Mtume Adam (a.s.) alimwambia Allah swt: "Ewe Mola wangu! Mimi nimeghalibiwa na Sheitani, naomba unijaalie jambo lolote lenye faida kwangu."Hapo Adam (a.s.) alijibiwa:"Ewe Adam! Ninakupatia jambo ambalo iwapo kizazi chako kitakapo kusudia kutenda dhambi, basi sitamwandikia dhambi lolote.Na iwapo atatenda dhambi moja, basi nitamwandikia dhambi moja tu.Na atakapo kusudia kufanya tendo jema, basi ataandikiwa jema moja.Na iwapo atatenda hilo jambo jema, basi ataandikiwa mema kumi badala yake."

Mtume Adam (a.s.) aliendelea, "Ewe Mola wangu:"Naomba unijalie neema zaidi.Allah swt akamjibu:"Ni neema kubwa kwake yule atakaye tenda dhambi na aniombe *TAWBA*, nitamsamehe."

Hapo tena Mtume Adam (a.s) akasema,"Ewe Mola wangu: "Naomba uniongezee" Allah swt akamwambia:"Ninakujaalia kwa ajili ya kizazi chako, *TAWBA* hadi kufikia pumzi ya mwisho.Na iwapo ataniomba *TAWBA* wakati huo wa mwisho wake,basi nitaikubalia na kumsamehe!"

Kwa hayo, Mtume Adam (a.s.) alisema: "Ewe Mola wangu! Haya yamenitosha."

Mtume Mtukufu (s.a.w.w.) amesema:
"Ikiwa mtu atakuwa amefanya *TAWBA* mwaka mmoja kabla ya kifo chake, basi Allah swt ataikubali *TAWBA* yake, na iwapo mwaka mmoja ulikuwa zaidi kwake, basi hata mwezi mmoja unatosha, na iwapo nayo ilikuwa mbali kwake, basi juma moja latosha, au hata siku moja pia inatosha kumfanya akubaliwe *TAWBA* yake kabla ya kifo chake. Na iwapo siku hiyo moja pia ilikuwa ni zaidi kwake, basi aombe *TAWBA* punde kabla ya kifo chake, na hata kama hivyo pia haitawezekana, basi aiombe *TAWBA* katika pumzi ya mwisho aipumuayo iwapo kooni mwake, basi Allah swt ataikubalia *TAWBA* yake." (Usuli Kaafi: Mlango wa *TAWBA*).

Allamah Majlisi (A.R.) anaelezea kwa kutilia mkazo Hadithi hiyo kuwa *TAWBA* itakubaliwa kwa kutegemea daraja za ukamilifu wake, kwa hivyo ifanywe kila jitihada ili kufikia daraja hizo na tuufanye moyo wetu uwe mweupe kwa nuru na matendo mema na vile vile nyoyo zetu ziwe nyenyekevu. Iwapo mtu hakuweza kufanya *TAWBA* katika kipindi cha mwaka mmoja kabla hajafariki dunia basi afanye hivyo katika kipindi cha mwezi mmoja. Na iwapo hakubahatika katika mwezi mmoja kabla ya kufariki, basi atubu kabla ya juma moja na kama hivyo pia hakuweza kubahatika, basi atubu siku moja kabla ya kifo chake au saa moja kabla ya kifo chake basi hapo Allah swt atamsamehe madhambi yake yote.

Lakini upo wakati (muayyan) ambao umezungumziwa katika Hadithi kwa ajili ya *TAWBA*, wakati huo *TAWBA* hiyo haitofaidisha chochote."

Sheikh Bahai (A.R.) anaandika katika kitabu chake 'Arbain' kuwa 'wakati muayyan' ni wakati ule ambapo mtu huwa anamwona Malaika (wa mauti).Na pia inawezekana kuwa wakati huo mtu anakuwapo katika hali ya maumivu (sakarati mauti) ya mauti na huwezekana kuwa hana fahamu timamu.Maulamaa wote wanaafikiana kuwa *TAWBA* ifanyiwayo wakati wa mauti ni bure na isiyoweza kumfaidisha.

Kwa hiyo ewe msomaji mtukufu, tufanye *TAWBA* bado tukiwa na fahamu zetu zilizotimamu, kwani isije ikatokea kuwa *TAWBA* yetu ingawaje tutaifanya lakini haitakuwa na faida yoyote kwetu!

Allah swt anatuelezea katika **Sura an-Nissa** Aya 17-18:-

"Toba inayopokelewa na Mwenyezi Mungu ni ya wale wanaofanya uovu kwa ujinga, kisha wakatubia kwa upesi. Hao ndio Mwenyezi Mungu huipokea TAWBA yao.Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi na mwenye hekima.

Hawana TAWBA wale ambao hufanya maovu mpaka mauti yamemhudhuria mmoja wao, hapo akasema: "Hakika mimi sasa natubu." Wala hawana TAWBA wale ambao wanakufa katika hali ya ukafiri. Hao tumewaandalia adhabu iumizayo. (***4:17-18***)

8. Kufanya Tawba Papo Hapo Ni Faradhi

Shaykh Bahai (A.R.) anaandika katika kusherehesha 'Arbain' kuwa: "Madhambi huenea mwilini mwa mtu kama vile sumu kali inavyoenea mwilini mwa mtu, basi juhudi za haraka sana zinavyofanywa kuzuia sumu isienee mwili mzima, ndivyo vivyo hivyo inavyotakiwa kufanya *TAWBA* ya madhambi yaliyokwisha fanywa ili maovu yake yasienee katika mwili mzima.Kuna hatari mbili ya kutokufanya *TAWBA*, kwanza iwapo atabakia hai, basi kuna uwezekano mkubwa kwake yeye kurejea katika madhambi aliyokwishayatenda na kuongezea mengine kwani alikuwa hakufanya *TAWBA*, pili iwapo atafariki (kwani hakuna anayejua wakati wake wa kifo) basi atakuwa amekosa hiyo fursa ya kufanya *TAWBA*, masikini huyo ataaga duni pamoja na mzigo wake wa madhambi akisubiri adhabu kali ya Allah swt."

Katika hali hii milango ya *TAWBA* na fursa zake zitakwisha kwa ajili yake. Allah swt anatuambia katika **sura Munafiqun**, Aya 10–11:

Na toeni katika yale tuliyokupeni, kabla mmoja wenu hayajamjia mauti,kisha akasema:"Mola wangu! Huniahirisha muda kidogo tu nikatoa sadaqa na nikawa miongoni mwa watendao mema?"

Lakini Mwenyezi Mungu hataiahirisha nafsi yoyote inapokuja ajali yake, na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote. (***63:10–11***)

Katika tafsiri ya aya hiyo, tunaambiwa kuwa mwanadamu wakati wa mauti yake huwa anamwambia Malaika wa Mauti kuwa ampatie muhula mdogo wa hata siku moja ili aweze kutubu madhambi aliyoyatenda, na ajiandae kwa ajili ya safari yake ya Akhera. Basi hapo Malaika Izraele atamwambia: "Siku za maisha yako zimeisha."

Hapo basi mwanadamu atasema:"Basi naomba muhula wa hata saa moja."

Atajibiwa:"Saa za maisha yako pia zimekwisha, na hapo pia umefungwa mlango wa *TAWBA* kwa ajili yako."Na hapo roho yake itatolewa –atakufa.Masikini mwanadamu huyo atafukiwa kaburini mwake akiwa bado amebakiza matumaini na mategemeo mengi, lakini yote hayo humo shimoni yatamsaidia nini? Katika hali kama hii, imani ya mtu ipo hatarini!

Jambo la pili ni kwamba, kwa sababu ya kutofanya *TAWBA*, kunatanda giza zito moyoni mwa mtu, na huendelea kupakwa giza zito ambayo haiwezi kamwe kutolewa.Kadiri atakavyokuwa akiendelea kutenda madhambi ndivyo utando huo mweusi utakavyoendelea kutanda juu ya moyo wake na hivyo matikeo yake ni kuendelea kutenda madhambi bila hata ya kujuta na kusikitika.Kwa mujibu wa riwaya, moyo kama huo unaitwa 'moyo mweusi.'

Imam Muhammad al–Bakir (a.s.) anasema:"Hakuna kitu chochote chenye kuuleta moyo madhara kuliko madhambi. Kila giza linavyozidi moyoni mwa mtu, hatimaye hulifunika lote kwa giza lake.Hapo ndipo

utamwona mtu anatoka kwenye nuru na kuingia katika giza na kupotoka kabisa kwani atakuwa haioni haki."

Katika riwaya nyingine, anasema Imam Muhammad al-Baquir (a.s.) kuwa: "Mfanya madhambi sugu kama huyu hataweza kutenda mema kwani mema yatakuwa yameshamwondokea zamani, na hivyo hadi kufikia mwisho wa maisha yake haweza kufanya *TAWBA*.Na iwapo atajaribu kufany *TAWBA*, basi itakuwa ni ya matamshi tu kwani moyo wake hautashiriki naye.Yaani yeye atatamka hivi na hisia zake zitasema vingine.Aina hii ya *TAWBA* haiwezi kuwa *TAWBA* halisi na wala haitakuwa na athari zozote.Mfano wake ni ule wa mtu kuzivaa nguo zilizo chafuka na huku akidai kuwa zimefuliwa.Kusema kwake huko hakuwezi kuzifanya nguo chafu zikawa nguo safi. Na mtu kama huyu anaweza kupotoka katika dini yake na wala dini yake haitamwathiri yeye. Mtu yeyote anapoiingiza imani yake katika hali ya hatari kama hii, basi ahera yake pia humharibikia."

9. Darja Za Tawba

Mbele ya Allah swt, *TAWBA* ni kule kunapomfanya mtu ajirudi (kutoka maasi). Hivyo wafanyao *TAWBA* ni wa aina zifuatazo:

1.Kurudia Imani kutoka kufuru,yakini kutoka shaka, kuelekea utoshe lezi kuacha kila akida za ubatili na kuingia katika haki.

2. Kuacha maasi na kuelekea katika utiifu na utekelezaji.

3. Kutoka katika maasi kuingia katika maarifa ya Allah swt na baada ya kupata maarifa kuwepo na ongezeko katika ibada.Na kama alikuwa ameghafilika, basi kuwepo na ongezeko la dhikiri. Nahivyo inambidi achukie kila aina ya dhuluma na badala yake apendelee uaminifu na utiifu.

Kwa mujibu wa vipengere hivyo hapo juu, imetuwia wazi kuwa *TAWBA* ni jambo lililo la lazima kwa kila mwanadamu kwa sababu inambidi awe katika hali ya kutokuwa na kulemewa na mzigo wowote wa madhambi.Na hii ndiyo hali ya maarifa na ibada ambapo mwanadamu huweza kujipatia daraja la juu mbele ya Allah swt.Ikiwa mwanadamu atajitahidi kwa kiasi gani kwa kujipatia maarifa, ibada na ushukuru, lakini bado tu hajaweza kujipatia maarifa kama inavyompasa. Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alikuwa mpenzi wa viumbe vyote, anasema: “Ewe Mola wangu! sikuweza kukujua vile ilivyokuwa ikinipasa kukujua na vile ilivyokuwa ikinipasa kufanya ibada yako, kiasi hicho sikuweza kukifanya!" Hayo ndiyo maneno ya Mtume (s.a.w.w.) ambaye alikuwa katika daraja la juu kabisa mbele ya Allah swt na mfanya ibada nyingi mno, mtoa shukurani mno, hata hivyo anaonyesha vile alivyokuwa akijihisi mbele ya

Allah swt.Mtume s.a.w.w. alikuwa akijiepusha hata na vitu vilivyo karahishwa (makruuh) katika sheria na vile vile alikuwa akijiepusha na vilivyokuwa mubah (matendo yasiyo na madhambi wala thawabu).Alikuwa mbora katika matendo mema. Mtume s.a.w.w. alikuwa amekamilika katika uwema na ucha Mungu.Amenakiliwa akisema:"Mimi huwa nasema 'Astaghfirullah' mara sabini kila siku (pasi na kifani)!"

10. Hali Ya Tawba Kamilifu Na Sunna Zake

Kama ilivyokwisha elezwa kuwa *TAWBA* ya hakika ni ile ambayo inayotokana na hisia tokea moyoni mwa mtu na kumfanya kujutia matendo yake aliyokwisha tenda.Vile itakavyokuwa masikitiko na majuto ya mtu, ndivyo *TAWBA* yake itakavyokuwa na ukaribu wa kutakabaliwa. Ikiwa mtu atahisabu dhambi zake kuwa ni kubwa sana basi ndivyo hisia zake za masikitiko na majuto yatakavyokuwa makubwa. Mfano wake ni kama ule wa mtu ambaye amekusanya mali yake yote aliyoichuma maishani mwake na kuchoma kwa moto.

Kwa hakika atajuta sana kwa hasara hiyo ya daima.Matatizo yake yataongezeka na hivyo majuto na masikitiko yake pia yataongezeka. Hivyo ndivyo ilivyo hali ya mtenda madhambi ambaye anajichomea mwenyewe na wala hakuna mwingine wa kumsaidia kwani moto huo upo umeshawashwa na Allah swt kwa uwezo wake na ghadhabu zake. Imam Ali (a.s.) amesema:"Haya ni matikeo ambayo haiwezi kustahimili ardhi wala mbingu, na joto lake si sawa na joto la humu duniani."

Imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema:"Iwapo mtu atatolewa kutoka Jahannam na kuwekwa katika tanuru lolote liwakalo humu duniani, basi humo ataishi kwa mustarehe kabisa kwa sababu kuungua kwa moto wa duniani si jambo la mushkeli, lakini hatuwezi kuustahimili moto wa Jahannam."

11. Uzani Wa Makosa

Mtenda madhambi haimpasi kulifikiria kosa lake kuwa dogo bali daima awe akifikiri kuwa amelitenda tendo au dhambi kubwa mno mbele ya Allah swt. Inambidi aelewe wazi wazi kuwa adhabu, ghadhabu za Allah swt ni kali mno kiasi kwamba hata dunia au mbingu haziwezi kustahimili.

Allah swt anatuambia katika **sura Buruuj** aya 12:

Hakika kutesa kwa Mola wako ni kukali sana. (***85:12***)

Vile vile katika **sura Muzammil**, Aya 12–13 twaambiwa:

Hakika tuna (***namna namna***) ***adhabu na moto uwakao*** (***mkali kabisa***). ***Na chakula kikwamacho*** (***kisakamacho***) ***kooni na adhabu iumizayo.*** (***73:12–13***)

Katika Aya hizi Allah swt anatuelezea ghadhabu na adhabu zake na shida zake, yaani kwa ufupi ni kwamba inambidi kila mtu awe akiyafikiria madhambi aliyoyatenda na awe daima akisikitika na kuhuzunika hadi mauti yake. Kilio na huzuni yake vitaweza kupooza miale ya moto ya Jahannam. Kilio chake kitaweza kuondoa giza lililotanda moyoni mwake.

Mtume Mtukufu (s.a.w.w.) amesema:
"Mwenye kutubu madhambi yake huwa sawa na asiyetenda dhambi kabisa (bali huwa bora zaidi ya huyo)."
(*Thawabul A'mal wa Iqabiha*. Uk. 273:*Tawba*)

Allah swt amesema katika **sura al-Baqarah**, Aya 222:

"Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa." (***2:222***)

Doa –I– Abu Hamza Thumali:
"Ewe Allah swt! Nijaalie *TAWBA* ile ambayo ni dalili ya mapenzi yako, na kwa kupitia *TAWBA* nikufikie hadi kwako!"

12. Kuzidi Kwa Masikitiko

Tawba Ya Mitume

Imeshadhihirika hadi sasa kuwa *TAWBA* sahihi ni ile ya masikitiko moyoni mwa mtu. Vile itakavyokuwa masikitiko yake zaidi ndivyo hivyo itakavyokuwa msamaha wa madhambi yake. Hivyo tuombe *TAWBA* zaidi ili madhambi yetu yote yasamehewe. Njia iliyo bora zaidi ni kuisoma Qurani Tukufu na kutafakari juu ya aya zake.

Khususan, inatubidi tusome visa vya Mitume a.s. na mafunzo yao, kama Mtume Daudi, Nuh., Yunusu, Yahya, Ayyub na tuone vile walivyokuwa wakilia ilhali wao walikuwa ni watu wasio na madhambi, bali walikuwa wakililia kuupata ule ukaribu wa Allah swt. Hivyo tusome visa vya wenye kufanya *TAWBA* na tujifunze kutokana nayo, tutawaleteeni visa kama hivyo hapo mbele.

13. Tawba: Saumu, Ghusli Na Sala

Kabla ya kufanya *TAWBA*, tutimeze aamali zifuatazo:
(a) Kufunga saumu kwa siku tatu:
Al-Imam Jaafer as-Sadique a.s. amesema kuwa Allah amewaamuru wenye kufanya *Tawba*tan-nasuha, kufunga saumu katika siku za Jumatano, Alhamisi na Ijumaa.
(*Wasail*, Kitabu Jihad,Babu 88, Uk. 363).

(b) Kufanya ghusli ya *TAWBA*:
Alikuwapo mtu mmoja ambaye alikuwa amejihusisha mno na matendo na ala za muziki. Siku moja alimwijia Imam ar-Ridhaa a.s. alimwambia:"Ewe Imam! Mimi nimekuwa mzoefu mkubwa wa nyimbo na muziki na ala zake, na sasa nataka kufanya *TAWBA*. Naomba uniambie nifanye nini. Imam a.s. alimjibu:"Amka na ufanye ghusli (kuoga kulivyoelezwa katika fighi)."

Mtume Mtukufu s.a.w.w. amesema:"Hakuna *TAWBA* iliyofanywa kama ipasavyo, na Allah swt asimsamehe mtu yanayoombewa *TAWBA*."Alimwambia mtu: "Iwapo utapenda kufanya *TAWBA*, amka, ufanye ghusli na kusujudu kwa ajili ya Allah swt."
(*Taharat, Mustadrak al-Wasail*, mlango 12).

(c) Kusali sala ya rakaa mbili au nne:
Imam Jaafer as Sadique a.s. amesema:"Iwapo mtu yeyote atapenda kufanya *TAWBA* kwa madhambi aliyokwisha tenda, basi kwanza atawadhe na kusali rakaa mbili na kumwomba Allah swt msamaha wa madhambi yake kwani yeye mwenyewe amesema katika **Sura an Nisaa** Aya 110:

Na mwenye kutenda uovu au akajidhulumu nafsi yake; kisha akaomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu ni mwenye kughufuria na mwenye kurehemu. (***4:110***)

Katika kitabu kiitwacho 'Iqbal' kwenye mlango wa matendo ya mwezi wa Dhilquada, kumeandikwa: Mtume Mtukufu s.a.w.w. alikuwa akiwaambia Sahaba wake siku ya Jumapili, kuwa, "Enyi watu! Je ni nani miongoni mwenu anayetaka kufanya *TAWBA*? Hapo Sahaba alianza kusema, "Sisi sote twataka kufanya *TAWBA*" Ndipo Mutume s.a.w.w. aliwaambia: "Kwanza fanyeni ghusli na kutawadha, salini rakaa nne. Katika kila rakaa baada ya Sura al-Hamur, someni Sura ya Ikhlaas na mara moja moja sura za Maudhtain, na baadaye fanyeni istighfaar mara sabini. Baadaye someni "*La haula walaa quwwata Illa Billahil 'aliyyil Adhiim'* na mkimaliza someni Dua yoyote. Lakini itakuwa afadhali iwapo mutasoma: "*Ya Aziiz, ya Ghafuuru, Ighfir dhunuubi*."

Iwapo mtu yeyote katika ummah wangu atafanya amali hii, basi mbingu itasema kuwa toba yako

imekubaliwa na umesamehewa, atasema Malaika mmoja juu ya ardhi. "Ziwe Baraka za Allah swt juu yako, vizazi vyako na ahali zako."Atasema Malaika mwingine: "Watu wasiokuwa radhi nawe,watakuridhia siku ya kiyama." Atasema Malaika mwingine: Ewe Mcha Mungu! Kaburi lako litakuwa salama na lenye nuru." Malaika mwingine atasema:"Wazazi wako wapo radhi nawe, nao wapo wameshaingia katika Rehema za Allah swt, na riziki yako itaongexeka hapa duniani na Akhera." Malaika Jibraili atasema: "Wakati wa mauti yako, mimi nitakuwa pamoja na Izraeli nikimwomba aichukue roho yako kwa upole."

Hapo Sahaba walimuuliza Mtume s.a.w.w.: "Ewe Mtume wa Allah swt! Je, iwapo mtu atapenda kuifanya amali hiyo mbali na mwezi huo wa Dhilquada?"

Hapo Mtume s.a.w.w. alimjibu: "Kama nilivyoeleza thawabu zake zitakuwa hivyo hivyo.Hayo ni mambo ambayo Malaika Jibraeli alinikumbusha usiku wa Miraji."

14. Istighfaar, Kurudia Tawba Na Alfajiri

(d) Kusoma Istighfaar:
Kuhusu *TAWBA* inatubidi tusome sana Duaa zilizofundishwa na Mtume s.a.w.w.na Maimamu a.s. Khususan Sahifai Sajjadiyyah au Sahifai Kaamila (Dua Na. 31 ipo imewekwa humu mwishoni juu ya *TAWBA*) na asome 'Munajaati Khamsatashara (munajaat kumi na tano) za Imam Ali a.s. katika Mafatihul Jinaan (funguo za Peponi). Katika duaa hizo tutaona vile *TAWBA* inavyoombwa na vile tunavyoweza kujihisi kimoyo wakati tuzisomapo.

(e) Kurudia *TAWBA* na Istighfar:
Imam Jaafer as-Sadique a.s. amesema:
"Mtume s.a.w.w. alikuwa akitubu kila siku mara sabini, ilhali yeye alikuwa hana madhambi."
(*Wasail*, Kitabu Jihad, mlango 92. uk. 367)

Kwa mtu atakaye ongeza zaidi *TAWBA* , basi siku ya Kiyama matendo yake mema yatazidi kupendeza. (usuli Kafi. Kitabu cha Dua na Istighfaar).

Imam Ar-Ridhaa a.s amesema:
"Mfano wa Istighfaar ni ule wa majani ya mti, ambayo hutoa sauti kwa sababu ya upepo, kwamba mtu atakuwa amemfanyia Allah swt masihara (utani) kwani huku ameomba *TAWBA* wakati bado yupo ameyashikilia madhambi."
(*Ulsuli Kafi*, Kitabu Duaa, mlango wa Istighfaar).

Imam Jaafer as-Sadique a.s. amesema kuwa Mtume s.a.w.w. hakuondoka katika kikao hata kikiwa kidogo kiasi gani, ila amefanya Istighfaar mara ishirini na tano.

(*Usuli Kafi*, Kitabu Dua, mlango wa Istighfaar).

Ipo riwaya nyingine isemayo kuwa Mtume s.a.w.w. alikuwa akitamka '*astaghfurullah*' mara sabini na *'Atubu Ilayhi'* mara sabini.

Sayyid bin Taus, ameandika katika kitabu chake 'Nahjul ad-da'awaat' kuwa imepokelewa riwaya kutoka kwa Mtume s.a.w.w. kuwa "Apatwapo mtu na shida na dhiki, basi asome mara elfu thelathini: "Astaghfirullah wa Atub Illayhi." Kwa hakika Allah swt atamwondolea shida na dhiki aliyonayo. Riwaya inaelezea kuwa hivyo imeshajaribiwa na ni yenye manufaa sana.

(f) Wakati wa alfajiri ni wakati bora kwa ajili ya Istighfaar:
Wakati wowote ni wenye manufaa sana kwa ajili ya *TAWBA*, lakini wakati wa *Sahar* (sehemu ya mwisho wa usiku hadi alfajiri) huwa na athari ya ajabu kwa ajili ya *TAWBA* yaani madhambi yake yote yatasamehewa kwa pamoja.
Qurani inatuambia katika **Sura ad-Dhaariyaat**, Aya 17 na 18:

***Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.Na wakiomba maghufira,* (*msamaha*) *nyakati za kabla ya alfajiri.* (*51:17-18*)**

Vile vile katika **sura Ali Imraan**, Aya 17:

***.....na waombao maghufira saa za kabla ya alfajiri.* (*3:17*)**

Imam Ali a.s. amesema:
Allah swt anapotaka kuwateremshia adhabu watu wa ardhini, husema: "Iwapo wasingekuwa wale wanaonitukuza, na wanao imarisha na kudumisha misikiti yangu na ambao wanafanya istighfaar wakati wa alfajiri, kwa hakika ningewateremshia adhabu yangu."
(*Wasail ash-Shia*, Kitabu Jihad, mlango 94, uk. 374)

Mtukufu Luqman alikuwa akimwambia mwanamke: "Ewe mwanangu mpenzi! Angalia kuku asije akawa mbora kuliko wewe,kwani yeye akaamka alfajiri na kufanya Istighfaar, wakati ambapo wewe bado umelala!" (*Mustadrakal- Wasail*, katika Wisaya Laqman).

Zipo Hadithi na riwaya nyingi zizungumziazo fadhila za kukesha alfajiri.

Katika Qunut ya '*Witri* (sala za *Tahajjud* au *layl*) ni kusema mara sabini '*Astaghfirullah*' na kusema *'Al-afwu'* mara mia tatu. Allah amemjaalia Mtume wetu Muhammad s.a.w.w. daraja la Mahmuud na hutimiza kila matamanio moyoni mwetu wakati wa alfajiri.

Kwa ufupi, wote wale waliotukuzwa na kupandishwa vyeo mbele ya Allah swt ni kwa sababu ya kukesha wakati wa alfajiri.

Kwa ufupi, wote wale waliotukuzwa na kupandishwa vyeo mbele ya Allah swt ni kwa sababu ya kukesha

wakati wa alfajiri.

15. Tuifaidi Tawba

Sisi tusiupoteze muhula huu wa *TAWBA* kutoka mikononi mwetu, na tusije tukaingia makaburini mwetu bila ya kufanya *TAWBA*, kwani huu ndio mlango wa Rehema. Neema hii ya *TAWBA* (kurejea katika haki) hubadilisha giza kuwa nuru, baya kuwa jema na vile vile kuuzima moto wa Jahannam. Iwapo utakufa huku umejitwisha mzigo mzito wa madhambi yako, utambue wazi kuwa kaburi ni mahala pabaya sana pa kutokewa adhabu.Lakini iwapo utakwenda huko umeshatubu, basi kaburi ni mahala pazuri kwa waliofanya *TAWBA*– wingi wa rehema. Shimo lako halitakuwa shimo la mateso, bali litakuwa ni mahala penye rehema!

Pale panapofikia maji, hugeuka kuwa kijani na hali ya uhai hujionyesha, na pale panapotokea machozi, hugeuka rehema. Iwapo mja ataka kumridhisha Mola wake, basi amrejee na kumlilia Mola wake. Yamebahatika yale macho ambayo hulia na kutoa machozi kwa khofu ya Mola na nyoyo nyenyekevu ni zile zilizojiweka chini (zisizo na kiburi, fakhari au maovu). Baada ya dhiki ni faraja. Amefarajika baada ya kufanya *TAWBA* ndiye mtu aliyebahatika mno!

Mtume Yusufu a.s. alikuwa ni Mtume na vile vile alikuwa ni mwana wa Mtume Yaakub a.s. alikuwa na sifa moja iliyo bora kabisa ambayo ni uvumilivu na saburi ya hali ya juu. Na hii ndiyo sababu alikubalia kuwasamehe kwa uwepesi ndugu zake kwa makosa makubwa kama hayo yaliyokuwa ametendewa nao.

Sisi pia tumwangukie Allah swt kwani atatusamehe madhambi yetu yote,Yeye atazikubalia duaa zetu zote, tuseme:"Ewe Allah swt! nilikuwa sijui, nilipotoka, nilikuwa katika ndoto na nilikuwa nimefungwa kwa minyororo ya matamanio ya nafsi yangu.

"Ewe Allah swt! Mimi nimekuwa nikiasi hukumu zako kwa kipindi kirefu mno, sasa nimeshaamka kutoka ndoto yangu.

Nisamehe harakati zangu zisizokuwa sahihi na kunifutilia makosa yangu yote. Ewe Mola wangu! Nisamehe makosa yangu. Ewe Msamehevu! Nisamehe makosa yangu! Kwani mimi nilikuwa mwovu na mtenda maasi, wakati wewe u Mrehemevu na Msamehevu na Makarimu, naomba msamaha! Niteremshee rehema na baraka zako ili niongoke kutokana na balaa za maasi."

16. Kilio Cha Mtubia Bora Kuliko Tasbihi Za Malaika

"Nyie nyote mmeketi hapa katika hali ya '*saumu* ' na joto kali, wazee na vijana wetu watakapoomba duaa katka hali hii, basi itakuwa na athari kubwa na sauti hizi tukufu zitafikia hata Malaika." Hayo ndiyo yaliyokuwa yamesemwa na Shahidi Mihrabu, mbele ya umati wa watu.

Hadithi Qudsi inasema:
Majuto ya mtu mwenye madhambi huwa ninayapenda zaidi kuliko nyiradi za wafanyao tasbini. Malaika hawana moyo uvunjikao, lakini mwanadamu huwa na moyo uvunjikao, lakini moyo huo unathaman kubwa sana mbele ya Allah swt. Mimi sielewi iwapo chombo kilichovunjika huwa kinaweza kuthaminiwa, kwani hupoteza uthamini wake, lakini kwa nini moyo unapovunjika huzidi thamani yake? Mwanadamu anapopatwa na msiba au matatizo basi hubahatika kuungana na dhamira yake na hapo huketi akijikumbusha madhambi yake na hatimaye huanza kilio chake mbele ya Allah swt kwa kutaka radhi zake. Huyo mwenye madhambi ni mtu mwenye hatia mbele ya watu lakini Allah swt anasema kuwa kilio chake humpendeza mno hata kuliko tasbhihi zao.

Je kwanini hatusemi:"Ewe Mola wetu! Mimi ninatambua vyema kabisa kuwa wewe unapendelea kilio cha mwenye madhambi ambapo mimi bado sijajitahidi kwa hayo? Ni aibu kubwa sana mbele yako!"

17. Allah Swt Huzikubali Tawba

TAWBA ni mojawapo iliyo dharuri, na ambayo utekelezaji wake ni faradhi kwa kila Mwislamu. Allah swt amesema katika **Sura an-Nuur**, Aya 31:-

Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu ili mpate kufaulu. (***24:31***)

Vile vile twaambiwa katika **sura an-Aam**, Aya 34:-

Mola wenu amejilazimisha rehema, kwamba atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujahili, kisha akatubu baada yake na akafanya wema, kuwa Mwenyezi Mungu atamghufuria kwani yeye ni mwingi wa msamaha na mwingi wa rehema. (***6:34***)

Allah swt anatuhumu katika **surat ad-Dhuaa**, ayaa 10:-

Wala usimkaripie aulizaye. (***93:10***)

Allah swt anatuhukumu sisi tusiwafukuze wale watuombao. Sasa itawezekanaje yeye akatufukuza jpale tumuulizapo jambo? Vile alivyotufanyia faradhi sisi ndivyo vivyo hivyo ilivyo juu yake kuyashughulikia maswala ya waja wake! Hivyo tusisite kumuomba kwani hataweza kuturejesha mikono mitupu! Kwa kifupi iwapo watagombana waja wawili basi itakuwa ni faradhi juu yao wote kutafuta ufumbuzi wa usuluhishi wao. Iwapo mmoja miongoni mwao atajitolea kwa ajili ya usuluhishi na uelewano basi ni faradhi juu ya mwenzake kukubalia usuluhishi.

Kufanya usuluhishi ni faradhi kwa wote wawili, atakaye tangulia ndiye atakayetangulia kuingia peponi.

18. Tuyateketeze Madhambi Yetu Kwa Tawba

Allah swt anatuambia katika **Sura Hujuraat**, aya 11:-

Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu. (***49:11***)

Sehemu hii ya mwisho wa aya hii inatubashiria na kutuitia katika *TAWBA* hivyo tuitikie mwito huo na tufanye *TAWBA*.

Allamah Iqbal anasema:"Matendo ndiyo yafanyayo maisha ya mtu yawe ya Peponi au Motoni, huyu kiumbe si wa peponi wala motoni alipoumbwa."

Enyi Waislamu! Njooni nyote mliokwisha yatumbukiza maisha yenu katika madhambi. Allah swt ametuambia sisi (49:11) tusiitane kwa majina ya utani na majina mabaya, na sisi hatukuyafuata hayo, je ni nani aliye na utulivu moyoni mwao kuwa wao hawakuwatazama watu wengine kwa mitazamo ya dharau na wala hawakuwaita watu wengine kwa majina ya utani na ya kubughudhi? Basi iwapo hiyo ndiyo hali yetu basi tuombe: "Ewe Allah swt! Kwa utukufu wa mwezi wa Ramadhani, kwa madhambi yote yaliyotendwa na ulimi wangu, ewe Mola wangu! Naomba ihsani zako juu yangu, kwanza, unisamehe! Pili, wale wote walio na haki zao juu yangu naomba waniwie radhi kwani inawezekana wakanijia siku ya kiyama na kunikaba shingo huku wakinidai kuwa, je wakumbuka wakati fulani ulituita kwa matani au ulitunyang'anya haki zetu? Ewe Mola wangu! Nakuomba kwa utukufu wako, unisamehe iwapo nimemtesa au kumtania mtu yeyote yule katika maisha yangu na umfanye huyo muumin aniwie radhi juu yangu. Ewe Mola wangu!"

Tuelewe waziwazi kuwa Allah swt ni Mkarimu mno na hazina yake haipungui, iwapo hatutatubu, basi sisi ni wadhalimu, kwani yeye daima ametuwekea wazi milango ya rehema. Iwapo mlaji ni mvivu na akabakia njaa, basi mwenye chakula ana kosa gani?

Wale wasiotubu ni madhalimu! Njooni iwapo sisi hatukumbuki chochote (tulichokitenda) basi Allah swt anakumbuka vyote, iwapo hatujui, basi matendo yetu yote yameshaandikwa katika amali zetu. "Ewe

Mola wangu! Iwapo nimetamka kwa ulimi wangu chochote kile chenye uchungu kwa muminiin au nimepoteza haki za Muumini au nimemkashifu, basi naomba msamaha wako kamilifu!"

Njooni tujitoe katika mipaka ya dhuluma na upotofu, na tusome dua ya Imam Zainul Aabediin a.s.: (Dua hii imechapishwa kwa ukamilifu mwishoni)

Ewe Allah swt! Natubia kwako kwa kila kitu ambacho kinapingana na Amri yako au ambacho kimepoteza mapenzi yako kwa kutokana na mafikirio ya moyo wangu, maono ya macho yangu na matamshi ya ulimi wnagu, kwa *TAWBA* kutokana na adhabu zako na kuponea kwa khofu ya maumivu ya ghadhabu zako kwa walio asi....."

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.w. amesema: "Iwapo mtu yeyote atamdhalilisha au kumkashifu mtu yeyote yule, basi Allah swt atamkasirikia mno." Hatujui kila kitakachowafikia wale waliomtesa Imam Husseyn a.s. na wafuasi wake, mateso ya kila aina. Wao walimwambia Imam Husseyn a.s akiwa katika kiu kikali cha siku tatu:"Ewe Hussein!Hebu tazama vile mto Furati (Euphrate) unavyopiga mawimbi, lakini hatutakupatia hata tone moja la maji kwa ajili yako au wafuasi wako."

Tujue kuwa Imam Husseyn a.s. alikuwa si pekee hapo Karbala (Iraq) bali alikuwa pamoja na wanwake na watoto wadogo wadogo na jamaa zake.

19. Tuombe Tawba Kwa Madhambi Tuliyokwisha Tenda

Haitupasi kamwe kumdharau mtu yeyote wala tusimfanyie masihara wala tusimdhalilishe kwani hatujui iwapo huyo mtu yu mwema nyuma ya pazia za macho zetu. Bali inatubidi tuseme, labda yeye anazo tabia njema kuliko tabia zangu ambazo mimi sinazo, inawezekana yeye anazo heshima zaidi mbele ya Allah swt. Vile vile inawezekana kuwa mambo yake usiyoyapendelea wewe yakawa ni mema: Huenda wakawa bora kuliko wao.

Katika maisha yetu, yapo maovu mengi mno, kuwadhania watu visivyo (kwa mabaya) na vile vile kumshuku Allah swt. Leo ni siku ya Ijumaa na ni tarehe 15 ya mwezi wa Ramadhani (hiyo ni siku ambayo Shahid Mihrabu Ayatullah Dastaghib Shirazi, alikuwa akiwahutubia waumini) ambavyo vyote ni tukufu, hivyo sisi sote (wake kwa waume) tulie sana katika kufanya *TAWBA* ya madhambi yetu yote na vile vile tule kiapo thabiti cha kutorudia kutenda madhambi maishani mwetu. Leo ni muhula wa *TAWBA*, na tuombe *TAWBA* tu, mauti ipo inatupigia hodi petu. Insha Allah, madhambi yetu yatasamehewa na pale tutakapokwenda mbinguni hatutakuwa na mzigo mzito tuliojitwisha wa madhambi.

Katika masaa ishirini na manne (24) huwa tunatumia masaa mengi katika kutenda madhambi, hata wakati wa kupumua pumzi pia huwa tunatenda madhambi. Hatuelewi hali yetu itakavyokuwa kwani huwa tunamshuku hata Allah swt na viumbe vyake, uwezo wa kupangiwa na kupanga maamuru ya mwanadamu. (*Qadhaa wa Qadr*), kwa hakika sisi hatumtakidi Allah swt kwa kukamilifu na hili ndilo dhambi kuu kabisa. Njooni tujumuike kuomba toba ya madhambi yetu yaliyopita na tuombe kuepukana nayo na tuseme kwa moyo wetu wote kuwa kuanzia sasa sisi hatutashuku matendo ya Allah swt na tujisalimishe mbele ya hukumu zake kwa kikamilifu.

Mwezi mtukufu wa Ramadhani unayo majina mengi sana, na jina mojawapo lililo mashuhuri ni 'mwezi wa Toba.' As shaikh as-Sadduq A.R. ameelezea kuwa Mtume s.a.w.w. amesema:

"Mwenye kuupata (aliyekuwa hai katika) Mwezi wa Ramadhani, na asisamehewe (madhambi yake katika mwezi) humo, basi huyo hana msamaha wa Allah."

Hadithi hiyo inatuelezea wazi wazi kuwa iwapo mtu hatasamehewa madhambi yake katika mwezi huu wa Ramadhani, basi hakuna mategemeo mengineyo tena ya kupatiwa msamaha. Katika usiku na mchana wa mwezi huu mtukufu huteremka rehema na baraka za Allah swt. Leo ni Ijumaa na tena ni siku ya kumi na tano ya mwezi huu Mtukufu, ni siku ambayo alimozaliwa Imam Hassan a.s. Tufanye Toba kwa wasila wa Imam a.s. aliyeuawa kwa kupewa sumu. Tusome Duaa za Istighfaar za Imam Zaynul Aabediin a.s. Sinabudi kuwaleteeni machache tu:

"Ewe Allah swt! Mimi nakuomba msamaha (toba) mbele yako kwa madhambi yangu yote yaliyo madogo kwa makubwa, yaliyo dhahiri na batini na yale yote yaliyokwisha pita."

20. Tusiwaite Watu Kwa Majina Mabaya Au Majina Ya Utani

Tusiwe na tabia ya kuwaita watu kwa majina mabaya na yale yaliyokuwa ya utani au mzaha. Mfano, iwapo mtu mmoja alikuwa 'Myahudi' hapo awali na baadaye akawa Mwislamu, basi haifai kamwe kumwita 'ewe mwana wa Kiyahudi.' Vile vile usimwite mtu 'mlevi' wakati amekwisha kufanya toba.

Ni lazima kabisa kuwaita Waislamu kwa majina yaliyo bora kabisa. Ni haramu kumwita Muumin kwa jina au sifa mbaya. Mfano "Ewe mfupi kama nyundo! au ewe "Mfasiqi' ni jina baya kabisa (kwa yeyote) baada ya yeye kuwa Muislamu.'"

Huyu mtu kwa sasa anayo imani na anatamka 'La ilaha illallah' Ole wenu iwapo mutamwita kwa kumnasibisha na kufuru. Laana ya Allah swt huwa juu ya watu wale wanaowasema waislamu kuwa ni

makafiri!

Kumwita mtu au kumwambia mtu kwa jina la fasiq ni haramu, bali majina ya kujitungia ya kila aina pia ni haramu ambayo humhuzunisha kila asikiaye. Popote pale anapoitwa Mwislamu ni lazima aitwe kwa majina mema na heshima sana. Ipo rewaya mojawapo inyosema kuwa alitikezea mtu mmoja mbele ya Imam a.s. na Imam alikuwa halijui jina lake, hivyo alimwita "Ewe uliye na bahati njema, je haujambo?

Ni lazima kabisa kuwaita Waislamu kwa majina yaliyo borakabisa. Ni haramu kumwita Muumin kwa jina au sifa mbaya. Mfano "Ewe mfupi kama nyundo! au ewe mrefu kama mnazi, au ewe kiziwi, ewe kipofu n.k. Hakika katika zama zetu hizi tabia hii imeshamiri mno, Allah swt anatuambia katika Sura Hujurat Aya 11:

"Enyi mlioamini! Wasije watu (***kikundi***) ***wakawachekea*** (***kikundi kingine cha***) ***watu*** (***kwa dharau***) ***ambao huenda wakawa ni bora kuliko wao; wala wasije wanawake wakawacheka wanawake wengineo ambao huenda wakawa bora kuliko wao na wala msitafutiane makosa miongoni mwenu na wala msiitane kwa majina mabaya*** (***ya kejeli***)***; Mfasiqi ni jina baya kabisa*** (***kwa mtu yeyote***) ***baada ya yeye kuwa Mwislamu; na yeyote yule asiyetubu*** (***kutubia kwa tabia yake hiyo***)***,basi hao ndio walio wadhalimu."*** (***49:11***)

21. Tawba Ni Faradhi Baada Ya Kila Dhambi

Katika faradhi mojawapo za Muislamu ni kutubia mara moja pala anapotenda madhambi na hivyo ndivyo ilivyo wajibu. Iwapo atamwona mtu mwingine akitenda madhambi, basi amshawishi kutubu. Mfano, unapoketi mahala fulani na ukaona kuwa mtu mmoja anamtania na kumfanyia masikhara mtu mwingine basi ni faradhi kwako wewe kumkataza huyo wa kwanza aache utani wake dhidi ya mtu wa jpili na papo hapo atubu, na vivyo hivyo ni faradhi juu ya mtu huyo wa kwanza kukubali nasaha yako na atubu papo hapo na iwapo hatatubia basi uendelee kumkumbusha kila mara umnasihi zaidi.Kwani ni faradhi kwako wewe kumnasihi na kwake yeye kutekeleza. Iwap yeye hatakubali basi Aya hii itakuwa ikimzungumzia.

Quran inatuambia "Dhalimu ni nani?" Basi dhalim ni yule mtu ambaye amekwisha tenda madhambi na asiye tubu mbele ya Allah swt na wala asimwombe Allahs swt msamaha wa makosa yake.

22. Tawba Ni Nuru Ya Matumaini

"Ewe uliyekwisha tenda madhambi! Usikate tamaa kwa rehema za Allahs swt, rejeeni katika njia yake, na hataki muendelee kutenda madhambi vile mupendavyo na mutakavyo – tukidhani kuwa atatusamehe tu! La sivyo hivyo! Makusudi ya kutokata tamaa ni kwa wale waliokwisha tenda madhambi wakidhani kuwa hawana la kufanya kusamehewa hivyo wakaendelea na maasi yao, bali inawabidi waitambuw na waombe *TAWBA* na msamaha wa Allah swt. Hivyo wajue kuwa pale wanapotenda dhambi, waombe Toba mara moja. Inawezekana Allah swt akazikubalia *TAWBA* zetu.

23. Kisa Cha Kijana Mwenye Madhambi

Ma'adh anasema: "Siku moja nilikuwa nkijiandaa kwenda kwa Mtume s.a.w.w. , na mara nikamwona kijana mmoja akilia mno, basi hapo nilimwuliza sababu ya kilio chake hicho. Huyo kijana alinibu kuwa yeye ni mwenye dhambi kubwa mno. Basi hapo nilimwambia aje pamoja nami kwa Mtume s.a.w.w. ili amwombee msamaha kwa Allah swt. Hapo huyo kijana alisema kuwa alikuwa akiona aibu kuja mbele ya Mtume s.a.w.w. kwa sababu ya dhambi zake." Hapo Ma'adh aliendelea na safari yake hadi kwa Mtume s.a.w.w. na kumwelezea yale yaliyotokea. Basi Mtume s.a.w.w.alimwambia akamlete yule kijana. Alipofikambele ya Mtume s.a.w.w. aliulizw, 'Je umekuwaje, walia kwa nini? Hapo huyo kijana akasema, "Ewe Mtume wa Allah swt! Dhambi langu ni kubwa mno!"

Hapo Mtume s.a.w.w.aliendelea kumwuliza, "Je kosa lako kubwa au mbingu? " Akajibu, 'Kosa langu!' 'Je kubwa au dunia nzima? Akajibu, kosa langu! Je kosa lako kubwa au msamaha wake Allah swt? Hapo huyo kijana akasita na hatimaye kukubali kuwa 'Msamaha wa Allah swt ni mkubwa! Bassi hapo Mtume s.a.w.w. alimwuliza, sasa niambie kosa lako. Huyo kijana akaanza kusema: "Ewe Mtume wa Allah swt! Palitikea kufariki kwa binti mmoja mzuri mno wa kabila la ansaar, na mimi nilikwenda usiku ule kulifukua kaburi ili kutaka kuiba sanda aliyokuwa amevishwa huyo maiti, shetani alinighalibu na kunifanya nikatenda tendo la kinyama kwa maiti huyo, binti aliyekuwa uchi mbele yangu. Hapo ndipo maiti hiyo ilipota sauti ya masikitiko na kunilaani kwa kuniambia kuwa Allah sw ataniingiza motoni na kuniunguza humo kuteketea. Ewe mtume wa allah swt kwahakika, baada ya matamshi hayo ya maiti huyo, mimi nimekosa furaha ya kila aina na nimeingiwa na woga na nadhani nitaweza kuangamia katika hali kama hii iwapo itaendelea kunisumbua.Hapo mtume s.a.w.w. alimwambia huyo kijana:"Ondoka haraka mbele yangu kwani inawezekana moto wa Jahannam ukanikumba nami pia." Je kwa nini Mtume s.a.w.w. alisema hivyo? kwa sababu dhambi lilikuwa kubwa mno!

Kwa mujibu wa riwaya, kijana huyo baada ya kuambiwa hivyo, aliondika akiwa amesikitika mno na kuelekea katika milima ya mji wa madina, huko alikaa kwa muda wa siku arobaini akiwa akilia na

kuomba Toba kwa Allah swt. Baada ya siku arobaini kupita, alisema: "Ewe Allah swt! Iwapo umeshakwisha kuikubalia Toba yangu, basi naomba unijulishe kwa kumpitia Mtume wako. Na iwapo bado haujaikubali Toba yangu, basi naomba uniteremshie miale ya moto kutoka mbinguni ili inichome na kuniunguza ili niteketee kabisa!"

Basi hapo iliteremka Aya ya 134 – 135 ya **sura Ali Imraan** (3)

"Na wale ambao, wanapofanya tendo la kuaibisha au kudhulumu nafsi zao,wakamkumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha wa madhambi yao, na ni nani awasamehee madhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? Na ambao hawabakii* (kwa kukusudia***) ***katika yale waliyoyafanya maovu hali walikuwa wakiyajua hayo,"***

Na kwa hao, malipo yao ni msamaha kutoka Mola wao na bustani chini yake kunapita mito, watamokaa milele; Na utukufu ni malipo ya wale watendao haki." (***3:134–13***)

Hapo Mtume s.a.w.w aliwauliza masahaba wake pale alipo huyo kijana mwasi wa Allah swt. Alijibiwa kuwa yupo katika mapango fulani ya milimani akiwa katika hali ya kufanya Toba na kuomba Allah swt msamaha wa dhambi yake. Mtume s.a.w.w. alimwendea huyo kijana na kumbashiria juu ya kukubaliwa kwa Toba yake.
Tuzingatie kuwa:–

Huyo kijana alijitenga na wengine akilia huko pangoni kwa muda wa siku arobaini akiomba Toba kwa dhati, ndipo alipokubaliwa Toba yake.

Sisi tusijipotoshe kwa kudhani kuwa tutakaposema mara tatu Astaghfirullah' basi Allah swt atatusamehe madhambi yetu na kuikubalia Toba yetu,

24.Toba Inaweza Kukubaliwa Kwa Kumtawasuli Imam Hussein

Sisi huwa daima tunaomba, "Ewe Mola wetu! Tujaalie Tawfiqi ya Toba ili tuweze kusamehewa madhambi yetu na kiza cha moyo wetu kuondoka."

Wakati tuombapo, huwa hatujui iwapo dua yetu ni *Tawba*t Nasuuha au imekubalika kutufanya tusamehewe madhambi yetu yote. Hapo hapana haja ya kuhangaika kwani inatubidi kulia sana na vile vile kumtawasuli Imam Husseyn a.s. kwa kuomba msamaha wa madhambi yetu. Ipo riwaya isemayo kuwa,moyo wowote ule ulio katika hali ya kuhuzunika kwa mateso yaliyompata Imam Husseyn a.s na ahali yake na wafuasi wake, basi Allah swt huirehemu kwa baraka za Imam Husseyn a.s Imam Jaafer

as-Sadiq a.s amesema:"Atakayemkumbuka Imam Husseyn a.s. na kutokwa na machozi walau kidogo sana, basi atapewa malipo yake kutoka kwa Allah swt na ataridhiwa Jannati (peponi)! (Thawabul a'amaal Na. 631 aya ya 2) Lakini kumlilia Imam Huseini a.s. peke yake haimaanishi kuwa ni uokovu, bali itatubidi kujibu maswali juu ya haki za watu,madhambi makuu hadi hapo tutakaponuia kwa moyo thabiti wa kuacha madhambi na kutenda mema ndipo tufanye Toba kamilifu.Baadhi ya riwaya zinadema kuwa madhambi yote yatasamehewa ila madhambi makuu. Madhambi hayo makuu kamwe hayataweza kusamehewa ila kwa Toba kamilifu.

Na hii ndiyo maana Allah swt amechukua ahadi ya *TAWBA* tu:

Kwa hakika, Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote kwa pamoja (***Suraaz-Zumar,39:53***)

Na rejeeni kwa Mola wenu… (***39:54***)

Kwa hivyo kutokana na *tawassul* au Shifa'a kunaweza kusamehewa madhambi ili mtu asiseme kuwa yeye anayo madhambi mengi na hivyo ataingia Motoni tu, hivyo inambidi atambue wazi wazi kuwa kuomba msaada wa Imam Husseyn a.s.kutamfanya kusamehewa madhambi yake na hivyo inambidi awe mwenye kutegemea msamaha wake Allah swt.

Inambidi kila mtu ajiepushe na mapotoshi ya shetani kwa kila hali na hivyo tujitahidi kufanya Toba. Iwapo baada ya juhudi zetu hizi kutabakia kasoro zozote zile, basi Allah swt atatusamehe kwa msaada wa Mtume Mtukufu s.a.w.w. na Ahali yake watukufu a.s.

Hapa nitapendekeza kusomwa kitabu kilichoandikwa katika lugha ya Kiswahili: **'UPOTOFU WA MADHEHEBU YA 'WAHHABI' NA HATARI ZAKE.**' Kilichoandikwa na Khalifa M. Hamisi Mohammad na kinaweza kupatikana kwa anwani hii: Sherman Islamic Book Stall P.O.Box 5444 Dar es Salaam Tanzania E.A.

Katika kitabu hicho utaweza kusoma mengi pamoja na: Maana ya *Wasila, Itsighatha* (kuomba msaada kwa viumbe): Tawasul; kumzuru Mtume s.a.w.w. Madina; Mtume s.a.w.w. yu hai kaburini mwake; kuomba 'SHAFAA' (yaani kuombewa) siyo Shirki.

Vile vile ni muhimu kukisoma kitabu kiitwacho ***uchunguzi juu ya Uwahhabi*** kilichotolewa na Ahlul Bayt (a.s.) Assembly of Tanzania P.O.Box 75215 Dar Es Salaam – Tanzania. Kwa hakika kitabu hiki kinachambua masuala mengi mno na kwa undani.

Ama kuhusu ***Asili na kuenea kwa Uwahhabi*** jipatie kitabu hicho uweze kuelewa kwa undani kuhusu historia ya Mawahhabi.

Kwa hakika vipo vitabu vingi mno vinavyozungumzia upotoshi na mazushi ya Mawahhabi. Wasiliana na Bilal Muslim Mission of Tanzania P.O.Box 20033 DSM.

Ningalijaribu kuyadondoa machache hapa lakini itahitaji nafasi kubwa na si rahisi kuchukua machache

kuyaacha mengi yaliyomo.

25. Moyo Wa Sheitani Hubabaika Kwa Istighfaar Za Watu

Iwapo mtu yeyote anataka kupigana na adui shetani, basi itambidi awe na silaha gani? Mtume Mtukufu s.a.w.w. anatuelezea amali mojawapo ambayo inaweza kumvunjia sheitani juhudi zake zote. Nayo ni ISTIGHFAAR (kutubu) ambayo inamfukuzia mbali shetani. Je ni nani miononi mwetu ambaye hajawahi kumtii na kumfuata sheitani? Wingi wa wakati wetu wa magomvi huwa tunamtii sheitani, je hasira na ghadhabu zetu zisizo na msingi au kutokuwa na huruma, si vyote hivyo ni vishawishi vya shetani?

Njooni nyote tutubu madhambi yetu yaliyotangulia na tumtii Allah swt na tumsujudie kwa utiifu. Allah swt anasema: **Sura an-Nisaa**:69

***"Hao watakuwa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu: Manabii, walio wa kweli* (*siddiqiina*)*, na mashahidi na salihiina* (*walio katika haki*)*, na watukufu ndio hao kama rafiki zao."*(*4:69*)

Inawabidi wanawake wafuate maisha ya Bibi Fatema az-Zahra a.s., binti yake Mtume Mtukufu s.a.w.w. na vile vile wanaume wafuate maisha ya Sayyidina Ali a.s.

"Wanaume ambao si biashara wala kuuza kuliko wapotosha ukumbusho wa Mwenyezi Mungu na kusimamiusha sala na kutoa Zaka: Wao waiongopa siku ambapo nyoyo na macho vitajinyonga kwauchungu." (*24:37*)

26. Wenye Kutubu Hawatatoa Ushahidi Dhidi Ya Madhambi Yao

Ni jambo la kusikitisha mno kuwa sisi na nyinyi tutasimamishwa kwa pamoja mbele ya Allah swt kwa ajili ya kutolewa uamuzi baina yetu kuhusu matendo yetu. Imam Jaafer as-Sadique a.s. katika Usuli Kafi, mlango wa *TAWBA* anatubashiria kuwa:

"Iwapo mtu atafanya Toba basi hilo jambo litambusuru siku ya Kiyama na wala halitapingwa na Malaika

waandishi wa amali zetu. Na iwapo huyo mtu hakufanya *TAWBA* maishani mwake, basi ataambiwa aelezee hesabu yake kwa ukamilifu, ambapo kama yeye alifanya *TAWBA* maishani make, basi Malaika watasema 'Ewe Mola wetu! Huyu mtu alikuwa akitamka kila mara Astaghfurullah na alikuwa akiomba *TAWBA* kwako!"

Allah swt anatuambia katika Quran Tukufu sura **Furqaan** Aya ya 70:-

***..Hao* (*waliotubia*) *ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema.....'*(*25:70*)**

Midomo ya watu wengine itabakia kimya wakati wa kuulizwa maswali na majibu kwani hataweza kujitetea, lakini midomo ya Muumin haitabakia kimya kwani daima husema: *"Lailaha Illallah haqqan haqqa ta'abbudan wa riqqan limaanan wa tasdiiqan.'*

Mwenyezi Mungu anatuambia katika sura Yaasin aya 65:

***..Katika siku hiyo sisi tutaweka mihuri* (*tutaviziba*) *juu ya midomo yao ..... .*(*36:65*)**

Watu ambao daima walikuwa wakisema uongo na upotofu katika maisha yao,basi siku ya Kiyama ndimi zao zitakuwa bubu kwani watashindwa kutamka lolote na hapo viungo vyao vya mwili wao vitasema na kutoa ushahidi dhidi yao. Allah swt atujaalie tawfiqi (uwezo) wa kufanya Toba kabla ya kufariki kwetu! Aamin.

27. Viungo Vya Mwili Vitatoa Ushahidi Dhidi Ya Madhambi Yetu

Baadhi ya Maulamaa wameelezea ushahidi utakavyokuwa wakati wa Qiyama ambapo sehemu zote na viungo vyote vya mtu vitatoa ushahidi.Allah swt anatuambia katika **sura ar-Rahmaan**, Aya ya 41:

***"Wenye hatia* (*wenye madhambi*) *watatambulikana kwa alama zao, na wao watakamatwa kwa nywele za utosi wao na miguu yao."* (*55:41*)**

Mfano wake ni kwamba atakapotokea mtu ulimi wake umening'inia nje ya mdomo wake huku umebanwa na meno yake ya juu na chini na mdomoni mwake kunatoka miele ya moto, na huku damu na usaha unadondoka, basi atajulikana kuwa huyo alikuwa ni aalim (aliyepata elimu) aliyekuwa akizungumza maneno yenye nasiha kubwa kubwa bila ya yeye kuyatekeleza aliyokuwa akiyasema na vile vile alikuwa ni msema uongo. Vile vile ataonekana mtu mwenye tumbo kubwa mno kiasi kwamba hawezi hata kutembea, basi huyo atajulikana kuwa ni mwenye kupokea ribaa na kuifanyia biashara yake.

Allah swt anatuambia katika **sura al- Baqarah**, Aya ya 275:

***Wale wanaokula ribaa, hawataweza simama* (*siku ya kiyama*) *ila kama yule aliyesimama ambaye ametunduwazwa na mguso wa shetani."* (2:275)**

Udhahiri wa mtu siku ya kiyama utaonyesha madhambi aliyokuwa akitenda akiwa humu duniani. Iwapo kipaji chake kitakuwa na nuru basi atajulikana kuwa huyu alikuwa ni mfanya sujuda nyingi wakati akiwa humu duniani. Wenye kusujudu watakuwa wakitokwa na miale ya nuru kutoka vipajini mwao, au yatatoa ushahidi wa kutenda kwao matendo yao katika mikono yao ya kulia, basi hayo yatatoa ushahidi wa kutenda kwao matendo mema.

Allah swt anatuambia katika Quran, **sura Yaasin**, Aya ya 65:

***ituzungumzie mikono yao na itoe ushahidi miguu yao .....* (*36:65*)**

Maulamaa wanasema kuwa ushahidi wao utatokana na viungo vyao na ushahidi huo (**Ar-Rahmaan**: 41) utakuwa,lakini ushahidi thabiti utakuwa ni ule ambao utatolewa na viungo vyao -mikono na miguu itasema. Na uthibitisho wake wa wazi ni Aya hii:

Na wao wataziambia ngozi zao: "Kwa nini mnashuhudia dhidi yetu?" Hizo zitajibu: "

***Ametufanya Mwenyezi Mungu tuseme, ambaye amekifanya kila kitu kiseme....."* (*41:21*)**

Wakati sehemu zote na viungo vyote vya mtu vitakapoanza kusema kila kitu bila ya kuficha, hapo huyo mtu masikini atasema,"Je kwa nini mnazungumza dhidi yetu?" Basi hapo hivyo viungo vitasema: "Sisi tumejaaliwa uwezo na Allah swt wa kuzungumza kama vile vilivyo jaaliwa vitu vyote viweze kuzungumza."

28. Mbele Ya Allah Swt Miguu Na Mikono Vitasema

Baadhi ya Mufassirina wanasema kuwa siku ya Kiyama kitakachoweza kusema ni mdomo tu, je viungo kama mikono na miguu vinaweza kusema?Wao wanasema kuwa hali ya udhahiri wa mwanadamu tu ndio utakaodhihirisha hali yake huyo mtu, na wala si mikono au miguu. Basi hao tunamwambia kuwa 'matamshi' si mahitajio ya ulimi bali ni Allah swt anayejaalia uwezo wa mdomo kutamka maneno. Kutamkwa kwa maneno ni Sifa ya Allah swt na wala si kasoro. Iwapo ingalikuwa hivyo, basi ng'ombe na punda pia wanayo midomo na ulimi hata mirefu kuliko wanaadamu. Basi imetuwia dhahiri kuwa mwanadamu amefadhilishwa na Allah swt kwa kumjaalia 'uwezo wa kutamka.' Katika neema kubwa

kabisa za Allah swt kwa mwanadamu ni akili, hivyo ulimi ni tafsiri ya akili ili aweze kusema. Wanyama hawajajaaliwa neema hiyo.

Watu wenye akili watambua kuwa 'utamkaji' hauna uhusiano hasa na ulimi, bali ni Allah swt tu aliyezijaalia ndimi za wanaadamu ziweze kutamka maneno. Siku ya kiyama, hata vidoke vyetu vitafanya kazi hiyo hiyo na kusema kuwa huyu mtu alimnyooshea kidole muumin fulani kwa dharau au aliandika kwa kalamu yake mambo dhidi ya muumin. Zipo riwaya zisemazo kuwa hata nywele za mtu pia zitatoa ushahidi wao dhidi ya mtu mwenyewe.

Dalili ya pili ni kule ambapo mtu hatakaporidhika pale viungo vyake na sehemu za mwili wake zitakapotoa ushahidi dhidi yake.Lakini hivyo navyo vitasema kwa kuwa vimejaaliwa Allah swt uwezo huo wa kusema.

Malaika wote wanao uwezo wa kuzungumza na vile vile viumbe vyote tusivyoviona pia vinao uwezo wa kusema:

.Na hakuna chochote ila kinamsabihi yeye (Allah swt). (17:44)

Baada ya kifo cha mtu, huwa anaelekea katika sehemu za Malaika.
Iwapo ungalikuwa nauwezo wakuyasikia yaliyoghaibu (yasiyoonekana machoni mwetu) Basi hata viungo vyako pia vinamtukuza allah swt, lakini hauyasikii.Mwanadamu hawezi kutambua kwa kuhisi tu kwani sisi tupo humu duniani na wala hatuna uwezo huo wa ziada. (Jikumbushe kisa cha Mtume Suleyman a.s.alipokuwa akipita penye makazi ya mdudu sisimizi).

Kinaadhimisha utukuzo wa Mwenyezi Mungu chochote kile kilicho mbinguni na chochote kile kilicho ardhini. (62:1)

Kesho siku ya *Qiyama*, Allah swt atakijaalia kila kiungo 'uwezo wa kusema,' na vyote vitasema kama kawaida.Dhambi hata moja halitafichika hata kama kikiwa kidogo kiasi gani, lakini iwapo tutakuwa tumeisha fanya Toba maishani mwetu, basi viungo na sehemu zetu zote za mwili hazitatamka chochote dhidi yetu wala kutushitaki.

Kwa kifupi, itakuwa ni aibu na udhalilisho mkubwa kwetu sisi kushitakiwa na viungo vyetu sisi wenyewe.Hivyo, ili kuepukana na udhalilisho kama huo inatubidi tuwahi kufanya Toba ya madhambi yetu yaliyokwisha tendwa kabla hatujafariki na kukosa fursa hiyo.

29. Tusome Tasbihi Kwa Vidole Kwani Vitatoa

Ushahidi Wake

Katika tafsiri 'Ruh al-Bayaan, kwa mukhtasari kuwa Mtume Mtukufu s.a.w.w. aliwaambia wanawake kuwa wawe wakisema kwa wingi sana tasbili.

Ipo riwaya nyingineyo isemayo kuwa Mtume mtukufu s.a.w.w. anasema:
"Usiku wa *Me'raj* nilimwona Malaika mmoja akijenga jengo. Alikuwa akiweka tofali la dhahabu na mara tofali la fedha, na mara nyingine alikuwa akingojea. Mimi nilimwuliza 'je kwa nini unangojea?' Alijibu: "Wakati mja wake Allah swt anapoanza Tasbihi, sisi huwa tunaanza kujenga jengo zuri sana, na mara anyamazapo, nasi pia twangoja.

Katika kipindi cha awali cha Islamu, hapakuwapo na tasbihi bali walikuwa wakihisabia kwa vidole vyao. Kuna vifundo vitatu katika kila kidole na hivyo kuna mafundo thelathini kwa jumla ya mikono yetu miwili. Hivyo tutoe tasbihi kwa kutumia vidole vyetu hivi. Amesema Mtume Mtukufu s.a.w.w."Toeni Tasbihi kwa vidole vyenu kwani siku ya Kiyama vitatoa ushahidi kwa kusema:"Ewe Allah swt! huyu mtu alikuwa akitoa tasbihi pamoja nasi."

Tasbihi kwa mara ya kwanza ilifanywa na binti wake Mtume Mtukufu s.a.w.w. Bibi Fatemah Zahra a.s. Yeye alipokuwa amekwenda kuzuru kaburi la Bwana Hamza, alirudi na udongo mchache na ambao aliutumia katika kutengenezaea Tasbihi.Alitumia hiyo tasbihi katika dhikiri ya Allah swt.

Katika kipindi cha Imam Jaafer as-Sadique a.s. alitilizia mkazo wa kutengeneza tasbihi kwa udongo wa Karbala. Iwapo tasbihi iliyotengenezwa kwa udongo wa Karbala ikizungushwa mkononi tu, basi inayo malipo makubwa kwani udongo wenyewe upo unafanya tasbihi.

Allamah Sheikh Shushtary anasema:"Tasbihi iliyotengenezwa kwa udongo wa Karbala, si tasbihi ya kawaida, bali inayo thawabu nyingi kupita kiasi na inazo khususi kwani ardhi ya karbala ni kipande cha peponi (Jannati)."

Imam a.s. alimwambia Sahaba wa Mtume Ja'abir:
"Ewe Ja'abir ! Uwe ukimzuru Hussein huko Karbala kwani Karbala ni kipande miongoni mwa vipande vya peponi (Jannati)."

Msomaji anombwa kurejea maudhui haya ya kusujudia juu ya udongo. "Kwa nini Mashia husujudu juu ya judongo" cha Bilal Muslim Mission of Tanzania P.O.Box 20033 Dar es Salaam Tanzania East Africa na 'Assujuud' ala turbatil Husseyn Inda As-Shiah al-Imaamiyah' (kiarabu) cha Sheikh Abdul Husseyn al-Amiini.Kilichochapwa na Dar az- Zafra, Beirut Lebanon.

30. Je Tawba Iweje?

Kufanya *TAWBA* ya Allah swt ni jambo la daraja la juu, na iwapo jambo hili likiandikewa kitabu kwa ufafanuzi zaidi, basi kitatokezea kitabu kikubwa mno, lakini sisi hapa tutajaribu kuelezea vile *TAWBA* inavyotakiwa kufanywa. Iwapo mtu atatokezea kusema kuwa ,mimi nimefanya *TAWBA*, nimehuzunikia na kusikitikia madhambi yangu, na vile vile nimeomba msamaha wake Allah swt lakini moyo wake haukusikitika au haukuhuzunika na wala hakuacha kutenda matendo ya madhambi. Basi watu kama hawa hawatafaidika kamwe na faida za *TAWBA* zisizo za Nasuha.

Al– Imam ar–Ridhaa a.s. amesema:
"Iwapo mtu atatamka '*Astaghfirullah*' ya moyoni, basi atambue kuwa amemfanyia mzaha Allah swt."

31. Majuto Ya Moyoni Yawe Kwa Ajili Ya Allah Tu

Iwapo mtu atasema kuwa mimi nimekwisha fanya *TAWBA* na huku moyoni hana majuto yoyote ya madhambi, basi huyo ni MWONGO. Kwani uhakika wa *TAWBA* ni kujuta kwa madhambi aliyoyatenda mtu. Inawezekana mtu akajuta au kusikitika kwa dhambi alizozitenda na wala majuto yake si kwa ajili ya kutaka kufanya *TAWBA* na vile vile mtu anaweza kujiepusha na matendo ya madhambi kwa sababu za kidunia tu kama vile anahofia asidhurike kwa hasara za kimwili au heshima yake itapotea kwa kujihusisha navyo au anaogopa asije akafungwa jela. Sasa iwapo yeye atasema 'Astaghfirullah' kwa kutokana na vitisho kama hivyo, basi huyo ni *mnaifki* na ndiyo maana tunasema kuwa yu–mwongo. Sifa kubwa kabisa ya *TAWBA* ni kwanza kuacha kutenda madhambi na kufanya majuto na huzuni kwa madhambi yaliyokwisha fanywa hapo awali.

Lakini kwa kuwa kilio chake ni kwa sababu ya khofu ya adhabu au kukosa thawabu za Allah swt basi ni sawa na yule mtu ambaye baada ya kutesa na kudhulumu kupita kiasi na yupo anatafutwa na Serikali kwa kushitakiwa ili akamatwe popote pale alipo na hatimaye kufungwa jela. Sasa anatumia hila kwa kumwendea aliyemdhulumu ili amsamehe huku akilia ili kwamba asije akakamatwa na polisi akahukumiwa. Haya hayakuwa matendo yake yenye nia njema ya kumwomba msamaha wa kweli bali yalikuwa ni baada na kwa khofu ya polisi.

Hivyo huyo mtu akiwa amejaa khofu ya Jahannam anafanya *TAWBA* – hadaa. Na iwapo angalikuwa na matumaini ya kutoingizwa motoni (Jahannam) basi asingalifanya *TAWBA* wala asingelisikitika na wala asingejitambua kuwa yeye ni mwenye madhambi. Swala hili lipo wazi na sisi hatuwezi kusema kuwa

hiyo ndiyo *TAWBA* hakiki. *TAWBA* ya uhakika ni ile ambayo itatoa ushahidi wa nia na matendo yake yaliyo mema na kumfanya mtu akajirekebishe na kufuata njia nyoofu.

Allamah Tusi A.R.na Allamah Hilli A.R. wameelezea katika 'Tajrid al-Kalaam' kwa mukhtasari kuwa, mtu aketi kwa kutulia na kusikitikia madhambi aliyoyatenda dhidi ya hukumu za Allah swt, basi hapo *TAWBA* yake inaweza kuwa sahihi.Lakini iwapo atafanya *TAWBA* kwa uoga wa serikali au kwa khofu ya kupoteza heshima yake mbele ya watu, basi *TAWBA* yake hiyo ni kujihadaa mwenyewe!

Hivyo tumeelewa kuwa *TAWBA* ni kwa ajili ya Allah swt tu kwani tumemwasi Allah swt na hivyo tunuie kuwa hatutarejea kamwe madhambi na hapo ndipo kweli tutakuwa tumefuata njia ya kufanya *TAWBA*.

TAWBA inayo mambo mawili, kwanza, kusikitikia na kuhuzunikia matendo maovu tuliyoyatenda, na pili, kunuia na kuazimia kutorejea kutenda madhambi na vile vile kujiepusha nayo.

Mtu atakapoukaribia wakati wake wa mwisho wa kufariki, na iwapo atafanya *TAWBA* au asipofanya, lakini ataingizwa kaburini tu.Iwapo atafanya *TAWBA* basi kuna uwezekano wa kupona adhabu za Jahannam, lakini Maulamaa wanapinga *TAWBA* ya wakati wa mwisho (sababu zake zitatokezea mbeleni). Firauni alitubu wakati wa mwisho wa maisha yake, lakini ilimfaidia nini? Alizama pamoja na wafuasi wake kwa pamoja.Hivyo nasi tusije tukatubu kumbe kutubu kwetu kusitufaidie chochote.

32. Mapenzi Ya Ahli Bayt Huelekeza Kwa Tawba

Watu wenye Imani na mapenzi ya Ahli Bayti Toharifu ya Mtume Mtukufu s.a.w.w. wanapotokezewa kufanya dhambi, basi ni rahisi kwao kujaaliwa tawfiki ya *TAWBA*. Allah swt kwa nuru na baraka za Mtume mtukufu s.a.w.w. na ma-Imam a.s.atawafanyia matokeo yao yawe mazuri.

Iwapo watu waliwafuata viongozi wa sini yetu kwa ukamilifu, wakatekeleza faradhi zao ipasavyo, wakajiepusha na yote yaliyoharamishwa, wakawafuata kikamilifu Ahli Bayt ya Nyumba ya Mtume a.s.na wakawa wakidumisha maulidi ya Husseyn a.s. basi siku ya kiyama Mtume s.a.w.w.atawasaidia wote.Wamebahatika wote wale watakaotetewa na Bibi Fatemah az-Zahra a.s. Wasio na bahati ni wale ambao hawana mapenzi ya Ahli Bayt ya Mtume s.a.w.w..

Pamoja na hayo, faida nyingineyo itokanayo na mapenzi ya Ahli Bayt a.s. ni kuondokana na ubakhili na huingiwa na moyo wa kutoa sadaka na misaada na hiyo ndiyo bakhshishi kubwa (lakini wale wasiotoa khums, zaka au sadaka na ambao hutoa rushwa na kukusanya mali kwa kutumia riba kwa hakika wao si wapenzi wa Ahli Bayt a.s.) Iwapo munataka kufanya mapenzi na Imam Ali a.s. na kumfuata basi muwajue hali mayatima, wajane, wageni na muwasaidie wenye madaris (wingi wa Madrassah au vyuo).

Wale walio wapenzi wa kweli wa Ahli Bayt a.s. kwa hakika hawawezi kufariki bila ya kufanya *TAWBA*.

Tawfiki hiyo Inshaallah watajaaliwa kabla ya mauti kuwafikia, na kuelekea peponi huku wakiwa hawana mzigo wa madhambi yao.

33. Tawba Ni Mlango Wa Rehema

TAWBA ni mlango mmoja mtukufu kabisa wa Rehema za Allah swt na *TAWBA* ni bahati ya watu wenye imani na wapenxi wa Ahli Bayt a.s. Tujue kuwa hakuna dhambi lolote lile lisiloweza kusamehewa, hata *TAWBA* ya Makafiri au mapagani pia huweza kukubaliwa.

Lakini mapenzi ya Ahli Bayt ya Mtume Mtukufu s.a.w.w. ni sharti mojawapo au sivyo mtu anaweza kukosaukubalio wa *TAWBA* yake hadi kufari dunia.Kwani mapenzi hayo yapo yameamrishwa na Mwenyezi Mungu katika Qurani Tukufu na vile vile Mtume Mtukufu s.a.w.w. pia ametulazimisha kwa hayo.

Ni lazima vile vile tutambue kuwa *TAWBA* itakayofanywa katika uhai wa mtu kabla ya kifo chake, ndiyo itakayomfaidi kwani atanuia kuacha maovu kuanzia hapo anapotubu lakini yule mtu anayefanya *TAWBA* wakati wa mwisho wa pumzi yake hutambua kuwa sasa hanao muda mwingine wa kutubu, hivyo anajaribu kufanya *TAWBA* ili anusurike, lakini hivyo haitamsaidia kwani anatambua kuwa hana njia nyingine ila ni *TAWBA* tu na hivyo hana wakati wa kujirekebisha na kuacha maovu kwani mauti imeshaanza kumtoa jasho utosini. Je, mtu kama huyo anaweza kudai kuwa hatarudia kutenda maovu tena? Ambapo katika *TAWBA* tunanuia kutotenda tena madhambi. Huyo amejihadaa kabisa. Watu kama hawa wapo wanzungumzwa katika Qurani Tukufu:

Na *TAWBA* (yenye faida) kwa ajili ya wale watendao maovu hadi mauti inapowahudhuria mmoja wao. (4:18)

TAWBA si jina la kulazimishwa, bali ni kutekelezwa kwa ibada zote zilizo za faradhi tulizoziacha, iwapo tunadaiwa fidia, basi tuzilipe na tuache kabisa mambo yote yaliyoharamishwa katika Islam.

Kwa kifupi ni kwamba, iwapo mtu ataathirika kwa masikitiko ya madhambi yake wakati wa kufa, basi haitambuliwi kuwa ni *TAWBA*. Kwani *TAWBA* ni kusikitika na kujutia kwa yale mambo yaliyo kinyume na maamrisho ya Allah swt na wala si kusikitika baada ya kuona na kuhisi adhabu.

Imam Zaynul Aabediin a.s. anasema katika Sahifa-i-Sajjadiyyah, kuhusu *TAWBA*:
"Mlango wa Rehema ulioufungua wewe (Allah swt) kwa ajili ya waja wako unaitwa *TAWBA*, mlango huo huwa daima upo wazi, sasa hakutakuwapo yeyote na kisingizio mbele yako...."

Allah swt anatuambia katika Qurani:

***Basi hoja yaMwenyezi Mungu* (*pekee*) *ndiyo amri* (*6:149*)**

Kwa yakini kuna ushahidi kamili mbele ya Allah swt, hivyo iwapo mtu atajaribu kujitetea visivyo kwa kusingizia kuwa alipotoshwa na matamanio nafsi yake, basi hapo atajibiwa:"Je, hatukuwawekeeni wazi mlango wa *TAWBA*? Sasa kwa nini haukufanya *TAWBA* na kuomba msamaha na rehema za Allah swt.

Bila shaka Rehema na Maghfirah za Mwenyezi Mungu zipo kwa wingi, hivyo inatubidi sisi tufanye *TAWBA* kamilifu ili maovu yetu yabadilishwe kuwa mema, kama vile Qurani isemavyo:

***..Hao* (*waliotubu*) *ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema.* (*25:70*)**

Kwa mujibu wa Aya hiyo juu ya sura al–Furqaan, si kwamba ni madhambi yetu tu ndiyo yatakayo futika bali hata matendo yetu maovu pia yatabadilishwa kuwa mema. Hivyo tujihadhari na jitihada za sheitani ambaye daima huwa akibuni kila aina ya mbinu za kuwapotosha wale walio katika Siraat–i–Mustaqiim.

Katika Sura an–Nahl twaambiwa:

***Kisha hakika Mola wako kwa wale wanaotenda ovu* (*tendo*) *katika hali ya ujahili* (*ujinga*) *na hugeuka* (*kwa kutubu*) *baada yake na hujirekebisha, kwa hakika Mola wako ni mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kurehemu.* (*16:119*)**

Katika tafsiri *'Majmaul Bayaan'* na *'Al–Miizan fi Tafsiril Quran'* Juzuu ya nne na Juzuu ya ishirini uk. 398 ya Allamah Syad Muhammad Husseyn Tabatabai. Chapa ya pili 1974 Beirut. Ipo riwaya ifuatayo juu ya *Istighfaar*:

'Baada ya kuteremka kwa Aya 3:135, Sheitani alikuja Makkah na kupiga sauti kubwa mno juu ya mlima Thuwayr, ambayo iliwafanya mashabiki wake wote wakusanyike, nao walipokuja walimwona bwana huyo amezongwa na mushkeli mkubwa sana na hapo hawakusita kumwuliza: "Je umekuwaje na hoja gani ya kutukusanya hapa?"

Akajibu: Imeteremka Aya isemayo kuwa Ummah wa Muhammad utasamehewa kabisa madhambi yake na masharti ya *TAWBA* yaliyokuwa yamewekewa Ummah yaliyotangulia, yameondolewa kwao. Na iwapo sisi hatukubuni mbinu dhidi yake, basi juhudi zetu zote za kuwapotosha hazitakuwa na athari yoyote kwani wao watakapofanya *TAWBA*,madhambi yao yatasamehewa yote kwa pamoja na hata kubadilishwa kuwa matendo mema."

Kwa hivyo nimekuiteni hapa ili tutafute mbinu za kukabiliana na swala hili ama sivyo sisi hatutakuwa na kazi yoyote ile."

Kila mmoja wao alitoa mpango wake aliinuka mmoja wa Masheitani, akasema: "Nitafanya hivi na vile....." Lakini hawakukubaliana naye, nao wengine pia walisema walivyokuwa wakiona, nao wote walikwenda wakipingwa mmoja baada ya mwingine.

Na hapo akainuka *Waswas – Khannas*, naye akasema: "Nitawatia watu katika hatia (madhambi) na papo hapo nitawasahaulisha Istighfaar (*TAWBA*) na nitawaambia kuwa "Ewe bado unao muda mwingi wa kufanya *TAWBA*, haraka ya nini? Huu ndio muda wako wa kustarehe na kufaidi umri wako! Siha yako na vile nguvu zako zinakuruhusu ufanye hivyo, hivyo starehe hadi utakapokuwa mzee, utafanya *TAWBA* kiasi utakacho!"

Kwa hayo, Masheitani wote walifurahi mno na yeye Khannas alikabidhiwa kazi hiyo hadi kufika siku ya Kiyama.
(Tafakari *Sura an–Naas*, Nambari 114)

Hizi ndizo wasiwasi za Sheitani ambazo huwapotosha watu wengi hasa vijana ambao hudhani kuwa wao bado wanao umri mrefu wakufanyw *TAWBA* hapo mbeleni. Sisi twachukulia uzee ndio wakati wa kufanya *TAWBA*, lakini nani anayejua kuwa uzee huo ataufikia au atakufa kabla yake. Je siku hizi hatuoni kuwa wazee ndio waliobakia hai ambapo vijana wamekufa kwa magonjwa kama UKIMWI? Na magonjwa mengine ambayo hayana hata muda wa kuyashughukikia vyema kama homa ya uti wa mgongo, (seven days) n.k. Kwa hivyo fanya lile uliwezalo leo badala ya kungojea kesho, kwani unaweza kuugua vibaya sana na hata kufa! Jambo linlotubidi kujiambia ni : "Sielewi ni lini mauti yangu itanifikia na kunichukua, labda hata sasa hivi ipo mgongoni mwangu ikinichukua, hivyo ni aibu kufika mbele ya Mwenyezi Mungu huku nimejitwisha mzigo mzito wa madhambi bila ya kufaidi fursa ya *TAWBA*!"

Je, ndugu zangu, Imani yetu haipo hatarini? Labda tukafa mauti isiyo ya Islam na ambapo Allah swt anatuambia tusife ile tukiwa Waislamu!

Quran Tukufu inatuambia katika **Sura ar–Ruum**:

"Kisha ubaya ndio ulikuwa mwisho wa wale waliotenda uovu, kwa kukadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu, na kwa haya walizoea kudhihaki. (***30:10***)

Vile vile twaambiwa katika Sura *Aali Imraan:*

Na harakisheni kwa (***njia ya kujipatia***) ***Maghfirah kutoka Mola wenu!*** (***3:132***)

34. Katika Tawba Ulimi Ndiyo Mfasiri Wa Moyo

Katika *TAWBA*, kama tulivyokwisha elezea hapo awali kuwa kitu cha lazima ni kusikitika na kuhuzunika kwa mtu, vile vile kujuta kwa moyo wake wote pamoja na kunuia kwake kuacha madhambi hayo na yote mengineyo. Na katika hisia hizo nzito atamke maneno mazito ya kuomba msamaha wa Allah swt na kusema: 'Astaghfirullah Rabbi wa atubu Ilayhi.'

TAWBA haiwezi kuwa *TAWBA* iwapo itatamkwa mdomoni tu bila ya kuwapo kwa hisia za moyoni. Hivyo inatubidi tuuelekeze ulimi wetu katika *TAWBA* baada ya kujengwa kwa hisia za moyoni kwani ulimi ndio utakao fasiri yaliyo moyoni mwetu. Ndipo hapo *TAWBA* yetu itakuwa ni sahihi.

Mfano, ninajuta na kusikitika kwa kusema matusi na maneno machafu moyoni mwangu, lakini ulimi wangu bado unaendelea na kuyasema hayo hayo. Basi katika hali kama hii, ulimi haujawa mfasiri wa moyo wangu. Utakuwa mfasiri pale utakapoacha kuyasema maneno hayo na mengineyo pia.

Hivyo tuombe Tawfiki ya kujaaliwa ulimi wetu uwe mfasiri wa moyo wetu ili kutukamilishia *TAWBA* kimoyo na kimatendo. Vile vile juhudi zetu pia zinahitajika, katika kujielekeza huko.

Ipo hadithi Tukufu isemayo:
"*Adda'i bila Aamal kar–raami bila watr*" Yaani:
Mwombaji bila matendo ni sawa na upinde bila kamba yake, au mti bila matunda, au mto bila maji.
Sasa tujiulize iwapo tutaomba tu bila kujitahidi wenyewe itakuwaje?

35. Kuiacha Tawba Na Kuendelea Na Madhambi

Imam Muhammad al–Baqir a.s. anaielezea 'kugang'ania hivi; katika Usuli Kafi:

"Iwapo mtu mmoja amefanya madhambi na wala yeye hanuii kuyaacha kabisa na wala hafikirii swala la kufanya *TAWBA*, basi kwa sababu hiyo itakuwa ni mazoea yake ya kutenda madhambu na hakutakuwa dawa nyingineyo yenye kuponya tabia yake hiyo ila *TAWBA* tu."

Maulamaa wengi wanaafikiana kuwa ni lazima kufanywa *TAWBA* papo hapo pale mtu anapotenda dhambi. Sheikh Bahi A.R. anasema kuwa mtu anazidi kujitwisha mzigo wa madhambi kila acheleweshavyo *TAWBA* kwani hiyo ni faradhi mojawapo na anastahiki kupewa adhabu kamili. Iwapo atafanya *TAWBA* kwa haraka basi atakuwa mustahiki wa rehema za Allah swt.

Ipo riwaya isemayo kuwa wakati mja anapotenda madhambi na kufanya *TAWBA* na tena akarejea kutenda madhambi na tena kutubu na kwa mara ya tatu tena akarejea kutenda madhambi na kutubu, basi hapo Allah swt anawaambia Malaika: "Enyi Malaika wangu! Angalieni vile mja wangu asivyoiacha nyumba yangu kwani yeye anatambua kuwa hakuna mwingine awezaye kumsaidia ila mimi tu!"

36. Tawba Ndiyo Sababu Ya Kusamehewa

Allah swt anatuambia 'Saabiquu' yaani haraka haraka mtangulie. Je ni wapi huko tena? Basi jibu ni kuelekea kwake Allah swt, hiyo *TAWBA* inaweza kuwa sababu ya rehema za Allah swt. Faradhi na Sunna zote ni sababu za rehema na Maghfirah za Allah swt. Matendo yote mema ni wasila wa Maghfirah zake Allah swt. Iwapo utauondoa mwiba njiani basi iwe ni kwa ajili ya Allah swt, na ulifanyalo jambo lolote lile, liwe kwa ajili ya Allah swt na yawe yote kwa ajili ya kutaka radhi na maghfirah zake Allah swt.

Katika baadhi ya kazi huwa tunababaika na baadhi huwa tunayo yakini. Lakini *TAWBA* ni tendo ambalo sisi tunayo yakini ya kutakabaliwa kwake na tukasamehewa madhambi yetu yote papo hapo iwapo tutaifanya kwa masharti na maelezo tuliyoyaelezea hapo awali.

Iwapo ulimdhulumu mtu na unataka msamaha basi lazima kwanza umwombe msamaha huyo mtu na iwapo atakusamehe ndipo hapo ujue kuwa umefaidika kwa kuupata Msamaha wa Allah swt. Allah swt anatuambia katika Qurani **Sura al-Baqarah**:

Na kuwa nyinyi wenyewe (***kwa hiari***) ***musamehe*** (***yote***) ***ni ukaribio kwa ucha Mungu*** (***Taqwa***). (***2:23***)

Msameheni kwa ajili ya Allah swt kwani yeye hupenda sana msamaha!

37. Mazungumzo Ya Imam Zaynul Aabediin Na Zahra

Imam Zaynul Aabediin a.s. alikuwa akielekea Makkah na aliliweka hema lake chini ya mlima mmoja ujulikanao kama 'Zahra.' Zahra alikuwa ni hakimu na pia alikuwa mfuasi wa Imam Zaynul Aabediin a.s. na alikuwa akimtembelea mara kwa mara.

Huyo Zahra siku moja alimhukumu mtu mmoja kifungo kwa makosa aliyokuwa ameyatenda, na kwa bahati mbaya huyo mfungwa alifariki akiwa kifungoni. Kutokana na tukio hilo, Zahra alijitoa hapo mjini Madina na kuishi katika mlima huo huu akilia na kujuta mno akiwa amewaacha mke na watoto wake wote.

Imam a.s. aliambiwa, "Zahra amevunjika moyo na kuwehuka na yupo daima akilia tu. Je, utapendelea kuonana naye kwani alikuwa ni miongoni mwa wakupendao wewe? Na Imam a.s. aliwajibu kuwa

angelipendelea kumwona na kujua hali yake.

Hapo Imam a.s. alimwendea huyo Zahra mlimani kwa kutaka kumpa mawaidha na hidaya. Zahra alikuwa uchi na katika hali ya kulia tu na alikuwa amedhoofika kabisa.

Riwaya inaendelea kusema kuwa Imam a.s. alimwambia: "Kutotegemea na kutarajia rehema na Maghfrrah za Allah swt kwenyewe ni dhambi mojawapo kuu hata kuliko tendo lako ulilolifanya. Sasa kwa nini hutaki kujitafutia njia ya kupona na hayo."

Hapo Zahra alijikaza na kusema, "Ewe bwana, je kunawezekana kukapatikana njia ya kuniponya na hayo niliyokuwa nimeyatenda kwani mimi nilimwua mtu katika hukumu yangu!"

Hapo Imam a.s. alimwambia: "Nenda kwa jamaa zake uwafidie na kuwaomba msamaha na urejee katika kazi yako hiyo hiyo kwani itakuwa na manufaa kwako humu duniani na akhera pia. Je, humu duniani kuna maumivu yoyote yale yasiyoweza kupatiwa ufumbuzi na matibabu yake? Inambidi kila mtu afanye haraka ya kufanya *TAWBA* na hii ndiyo njia ya kujipatia msamaha na rehema za Allah swt kwa haraka na urahisi wenye uhakika."

Njooni leo tufanye *TAWBA* kwa madhambi yote tuliyokwisha tenda na tunuie kutotenda tena madhambi yoyote yale.Tufanye *TAWBA* leo kwani mauti haina wakati.

38. Madhambi Ni Giza Wakati Tawba Ni Nuru

Allah swt anatuambia katika Qurani:

Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walio amini, yeye huwatoa kutoka giza na kuwaingiza katika nuru..... (***2:257***)

Imam a.s. anasema: "Kuongozwa kunamfanya mtu atolewe kutoka gizani na kuelekezwa penye maghfrah na ambavyo hatimaye *TAWBA* kamilifu."

Wale ambao wameshapotoka na ambao wanamfuata *Taaghuti* (sheitani) hutolewa kutoka nuru na kuingizwa katika giza. Hapa muradi (maanisho) ni wale ambao walikuwa katika nuru ya Islam na wakapendana na kiongozi mwovu na mdhalimu (sheitani) basi hao kwa sababu ya mapenzi hayo pamoja na mwovu wametoka kutoka nuru na kuingia katka giza. Basi hapo ndipo Allah swt anawaahidi kuwaingiza katika Jahannam pamoja na makafiri.

Mtu anapoamua kufanya urafiki wa Mwenyezi Mungu basi utamwona daima akijiweka katika hali ya tahadhari kwani utakachomwambia utaona akikuambia kuwa yeye kwanza atalifikiria na kuona iwapo

hakuna uvunjaji wa hukumu za Allah swt na vile vile ataangalia maadili. Kwa hakika katika mambo yako mengi wewe utamwona yeye akikuambia kuwa yeye hataweza kushiriki pamoja nawe katika safari, michezo au hata hafla fulani fulani na hata mikutano kwani sababu atakazokuambia wewe utaona kuwa huyu mtu amezidi mipaka ya ucha Mungu na hapo hautasita kumwambia kuwa 'Bwana, mambo haya unayotaka kufafuata ni ya kale, na dunia siku hizi imeshaendelea, hivyo achana navyo!' Lakini yeye hatatingisika katika uamuzi wake kwani yeye anataka ridhaa ya Allah swt! Na vinginevyo atakushauri wewe uyaache hayo kwani hayana faida kimaadili.

Lakini yule aliyejitakia urafiki wa Sheitani, mambo ni kinyume kabisa na hayo ya juu. Huyu hata bila ya kumwambia chochote utaona akibuni mambo ya kiajabu ajabu, mara hebu twende tukajaribu bangi, pombe, mihadarati, mabibi na maovu ya aina yote. Na wewe iwapo utajaribu kumpinga basi utaona akikulaumu na hatimaye ataweza kukushawishi kwa njia mbalimbali kwani atakuambia,"Basi twende pamoja, lakini wewe usifanye lolote lile" au mara nyingine "Twende lakini utajaribu kidogo tu na iwapo utaona haupendelei kuendelea, basi tutaacha na tutarudi....." Na hapo utaona kweli hebu niende na nitarudi iwapo sitapendezewa, lakini ukifika huko utaona akikugeuka na kukuambia ngojea kidogo tu, sasa hivi tutakwenda hebu jaribu kidogo....

Hii ndiyo tofauti kati ya nuru na giza, urafiki wa Allah swt na sheitani!

39. Madhambi Yote Yanaweza Kusamehewa

Katika Qurani Tukufu zipo aya nyingi mno na vile vile zipo hadithi ambazo zinazungumzia ukubaliaji wa *TAWBA* na vile vile zielezeazo kuwa madhambi yote yanaweza kusamehewa. Katika Qurani Allah swt anajisifu kuwa yeye ndiye Msamehevu na mwenye kuzikubalia *TAWBA* na vile vile anajiita katika Qurani kwamajina tofauti tofauti: Tawwab, Ghaffar, Ghafirudh–Dhunuub.....

Allah swt anawaita wale wote wafanyao madhambi wajirudi na kufanya *TAWBA* mara moja kabla hawajakumbana na adhabu zake zilizo kali kabisa. Suluhisho la daima la kuvunjika moyo, katika Sura az–Zumar:

***Sema** (**"Ewe Mtume Muhammad!**): **"Enyi waja wangu! Ambao mumezibadhirisha nafsi zenu, msikate tamaa ya rehema za Mwenyezi Mungu, kwa hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote kwa pamoja, hakika yeye ni Mwingi wa kusamehe, mwingi wa Kurehemu.** (**39:53**)*

Katika Aya hii Allah swt anawaita waja wake "Enyi waja wangu' na wala hakuwaita 'Enyi mlio asi' au 'Enyi wenye madhambi!' Na vile vile ametuusia sisi tusikate tamaa na kujidhulumu na badala yake anatupatia mawaidha ya kumrejea yeye ili aturehemu na kutusamehea.

Hivyo sisi tushikamane na imani yetu kwa Allah swt kwa maombi yetu na misaada yetu kwani ni yeye pekee awezaye kutusahilishia matatizo yetu. Yeye tu ndiye Tumaini letu.

40. Tawba Ya Mauaji

Iwapo mwuaji anataka kufanya *TAWBA*, basi inambidi kwanza ajisalimishe mbele ya warithi wa marehemu aliyeuawa na hapo ni shauri lao wao iwapo watatekeleza kisasi au watadai fidia au watamsamehe.

Iwapo mtu ataua kwa makosa au kwa kumdhania mtu kimakosa basi ni lazima kwake yeye kulipa fidia kwa familia na warithi wake marehemu. Na iwapo wao watamsamehe, basi ni faradhi juu ya muuaji kumfanya huru mtumwa mmoja, kuwalisha masikini sitini na kufunga saumu kwa siku sitini kwa mfululizo. Kama haweza kumfanya huru mtumwa mmoja, basi avitekeleze vilivyobakia.

Maelezo zaidi juu ya maswala kama hayo yanaweza kupatikana katika vitabu vya Fiqhi na Mafuqahaa wanaweza kutoa maelezo zaidi.

Tahadhari: Ni haramu kabisa kujitolea majibu ya maswala katika fiqhi tukisema: 'Kwa kuwa swala hili liko hivi, basi labda au bila shaka jibu lake litakuwa hivi na hivi.....' Hiyo ni Qiyaas, na qiyaas katika fiqhi ni haramu kwani itakuwa ni uamuzi usiofanyiwa utafiti.

41. Tawba Hutuepusha Na Moto Wa Jahannam

Imam Jaafer as-Sadique a.s. amenakiliwa riwaya moja katika *Usuli Kaafi:*
Siku moja Imam Ali ibn Abi Talib a.s. alimtembelea Sahaba mmoja na hapo alitokezea mtu mmoja akisema: "Ya Ali! Mimi nimetenda tendo la aibu pamoja na kijana mmoja (ulawiti), hivyo naomba nitakasike kwa mujibu wa Shariah za Allah swt."

Imam Ali a.s. alimwambia:"Kwa hivi sasa naomba uende zako kwani inawezekana ulitenda tendo hilo kwa ushawishi uliokuwa umekughalibuNa hivyo inawezekana kuwa akili zako hazikuwa timamu na maneno yako yasiwe yenye fahamu au maana yoyote."

Huyo mtu alirijea siku ya pili na kuyasema yale yale tena ya kutaka aadhibiwe.

Kwa mara ya pili, Imam Ali a.s. "alimwambia kuwa labda ulitenda katika hali ya ghadhabu ambayo ilikughlibu."

Aliporudia mara ya nne, Imam Ali a.s. alimwambia: "Mtume Mtukufu s.a.w.w. alitoa hukumu tatu katika sura kama hii, hivyo uchague mojawapo unayoipenda: (1) mikono na miguu yako ifungwe kwa pamoja na wewe utupwe chini kutoka mlimani, (2) Kichwa chako kikatwe kwa upanga na (3) Uchomwe mzima mzima kwa moto."

Hapo huyo mtu akamwuliza Imam Ali a.s..,"Je, ni adhabu ipi iliyo ngumu kati ya hizo tatu?" Na Imam Ali a.s. alimjibu, "Adhabu ya kuchomwa kwa moto." Na hapo huyo mtu alichagua kuchomwa kwa moto. Na alisema kuwa yu tayari kwa hayo.

Baada ya hapo aliondika, akaenda kusali rakaa mbili na akaanza kusema: "Ewe Allah swt! Mimi nilishawishiwa na hisia zangu za kinyama na dhamira yangu ipo ikinilaumu, nami ninaogopa madhambi na hivyo nimejileta mbele ya Mpenzi wa Mtume wako Muhammad s.a.w.w. ili yeye aniadhibu vilivyo kwa makosa yangu. Yeye amenielezea kuwa kuna adhabu tatu, nami, Ewe Allah swt! nimechagua ile ambayo ni ngumu kuliko zinginezo na ni matumaini yangu kuwa wewe U mkarimu na mrehemavu basi utanisamehe madhambi yangu kwa adhabu yangu hiyo ikiwa ni kaffar na utaniepusha na Moto wa Jahannam na ghadhabu zako."

Baada ya hapo alilia mno na kujielekeza katika moto. Miale ya moto yaliongezeka. Hapo Imam Ali a.s. pamoja na Sahaba wake walipoona hali hiyo, walilia mno. Na Imam Ali a.s. alisema: "Ewe mtu! Inuka, wewe umewaliza hata Malaika wa ardhini na mbinguni,yakini *TAWBA* yako imekubaliwa mbele ya Allah swt!"

Imam Jaafer as–Sadique a.s. amenakiliwa katika Bihar al–Anwaar cha Allamah Majlisi A.R. hivi:

Zipo mashua mbili zikielea majini mojawapo ipo imepakia shehena ya bidhaa na nyingine ipo tupu. Zinakaribia bandari ya nchi fulani na huko wanawakuta Maofisa forodha na kodi wakiwasubiri kupakua na kukisia kodi ya kuwatoza.

Je, mashua ipi itakayopita upesi bila ya kuulizwa maswali mengi na kufanyiwa upekuzi mkali? Bila shaka ni ile mashua isiyo na shehena ya bidhaa.

Mashua yenye shehena ya bidhaa itapekuliwa na kuhojiwa maswali mengi ya kila aina na bila shaka itachukua muda mrefu sana kabla haijaruhusiwa kuendelea na shughuli yake na kufika katika manxili yake. Na hapo watalipizwa kodi kubwa bila shaka na labda kupewa adhabu kali iwapo kutatokea hali isiyo halali.

Vivyo hivyo iwapo mtu atakufa huku akiwa ameshajitakasisha kwa kutimiza wajibu wake *TAWBA* basi siku ya Kiyama hatakuwa na muda mrefu wa kuhojiwa kwani atakuwa ametimiza wajibu wake humu duniani sala, zaka, khusi, saumu n.k. na vile vile amekuwa akiwatunza ahali yake, hakuwadhulumu wala kuwaonea watu, wazazi wake wamekuwa daima wakiangaliwa naye na kutimiza haki zao vile vile majirani wake na majamaa wake pia wamekuwa wakiangaliwa naye. Yaani kwa ufupi, amekuwa ni mwislamu mwenye kuzingatia maamrisho ya Allah swt wakati akiwa yu hai humu duniani. Basi mtu

kama huyo hatakuwa na mengi ya kuulizwa wala shida yoyote katika safari yake hiyo.

Vile vile ipo riwaya nyingineyo isemayo mtu kama huyo atakapoteremshwa kaburini kutakuwa kumejawa na nuru na atakuta kuna msafirishaji wake hapo na katika punde atajikuta yupo Jannati (peponi). Hapo wakazi wa Paradiso watamwuliza "Je, vipi mambo yako ya maswali na majibu yamekwendaje?" Na jee usafiri huu vipi? Basi hapo huyo atajibu: "Huu usafiri ni msikiti ambao nilikuwa nikiupenda mno nilipokuwa duniani na sasa umenifikisha hadi hapa Peponi."

Tuelewe wazi wazi kuwa Maasumiin–min –Allah ni shakhsiyyah wasiyo kuwa na madhambi na vile vile wale ambao watatenda mema na kufanya *TAWBA* ni sawa na watu wasiopata kutenda madhambi kamwe, hivyo ndivyo isemavyo Quran Tukufu na riwaya mbali mbali.

Na Allah swt amewaahidi watu kama hao: **Sura al–Furqaan**:

***…Hao* (*waliotubia*) *ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema……*(*25:70*)**

Kwa kifupi ni kwamba iwapo mtu atafariki dunia akiwa hana dhambi basi hatakuwa na maswali mengi ya kuulizwa na wala hatasumbuliwa popote pale katika safari yake hiyo. Iwapo mtu atakuwa amejitwisha mzigo mzito wa madhambi, basi atakuta maswali na mahojiano mengi yakimsubiri kwa muda mrefu katika Barzakh hadi hapo atakapotakasika kabisa na kuingia katika siku ya Kiyama.

Al–Imam as–Sadique a.s. amenakiliwa riwaya: "Mtu yeyote ampendaye Ali a.s. na kuwachukia maadui wake, na iwapo atakuwa amejitwisha mzigo wa madhambi bila *TAWBA*, basi huyo atabakia muda mrefu katika Barzakh akiadhibiwa hadi kutakasika kabisa. Atakapotokea siku ya malipo atakuwa hana la kujibu kwani atakuwa ametakasika."
(*Tafsir Nuru Thaqalain*, Kitabu cha tano, Uk. 165: *Tafsir Majmaul Bayaan*).

Imam a.s. alisema vile vile: "Mimi ninawakhofia mno adhabu za *Barzakh* (kizuizi) na siku ya kiyama tutawatetea waumini."

Hivyo inatubidi sisi tufanye *TAWBA* sahihi na kamilifu kabla ya kifo chetu ili tukifa tuwe ni waumini wa kweli ndipo tutakapopatiwa Shifaa ya Mtume s.a.w.w. na Maimamu a.s. kwani sisi tulivyo dhaifu hatutaweza kustahimili adhabu za mwenyezi Mungu na moto wa Jahannam. Tuelewe vyema kuwa huwa daima mauti inatufuata kama vile kilivyo kivuli chetu na labda muda huu tulio nao ndio wa mwisho, hivyo *TAWBA* ndiyo suluhisho letu la kuokoka humu duniani na vile vile Aakhera.

42. Msamaha Ndiyo Malipo Ya Istighfaar

Mfasiri mmoja wa Quran anasema:

a. Malipo ya *TAWBA* ni kukubaliwa kwake,
b. Malipo ya Istighfaar ni msamaha,
c. Malipo ya kushukuru ni kuzidishiwa neema,
d. Malipo ya Duaa ni kusikilizwa kwake,
e. Malipo ya sala ni kutimiziwa kwake,
f. Kwa kifupi Qurani inatuambia: Hakuna malipo ya wema ila wema tu! (55:60)

Aya hiyo ya Qurani ipo inazungumzia kwa ujumla na wala si kwa kitu maalum si muumin au kafiri. Hata hivyo madhumuni ya aya hiyo ipo imeelezwa na Imam Jaafar as-Sadique a.s.:"Iwapo mtu anakutendea wema, basi na wewe pia umtendee wema tu hata kama yeye atakuwa ni kafiri."

Ulifika wakati mmoja huko mjini Kufa (Iraq) ambapo mvua ilikuwa haikunyesha na hali ya hatari ilidhihirika na ndipo wakazi wa Mji huo walipomwendea Imam Ali a.s. na kumwomba aombe dua ya kunyesha mvua. Na hapo Imam Ali a.s. alimwambia Imam Huseyn awaombee dua ya kunyesha mvua. Na baada ya kuomba Dua, mvua ilinyesha na wakazi waliweza kutumia maji mengi hata katika kilimo. Lakini wakazi hao hao wa mji wa Kufa walimfanyia nini kwa malipo hayo ya ihsani aliyokuwa akiwafanyia kila leo?

43. Mazungumzo Ya Bahati

Imam Jaafer as-Sadique a.s. amenakiliwa katika *Usuli Kafi* akisema:
Mcha Mungu mmoja na fisiqi (mwenye madhambi) mmoja waliingia Msikitini kwa kufanya ibada. Walipotoka nje mambo yakawa yamebadilika kabisa yakawa kinyume.Yaani yule fassiq alipoingia Msikitini alivutiwa na ibada za huyo Mcha Mungu na hivyo aliathirika mno moyoni mwake. Hapo allah swt alipendezewa mno na hali yake hiyo. Lakini yule Mcha Mungu aliyekuwa anayo ghururi (majivuno) alipomwona yule Faasiqi huyu amejiingiza humu Msikitini miongoni mwetu sisi wenyewe kufanya ibada bora?"

Katika hali hii ya kiburi na majivuno alijiona kuwa yeye yu bora kuliko wengine. allah swt hakupendezewa na tendo hilo la majivuno ya huyo mtu, na hivyo akajikuta amejipotezea malipo ya matendo yake mema kwa sababu ya kiburi.

Allamah Majlisi A.R. anaandika:"Katika ukoo wa Bani Israeli alikuwa mtu mmoja Faasiq aliyekuwa akiitwa 'Khalii' (mwenye madhambi au aliyeasi).Basi huyo fasiqi alimwendea mcha Mungu mmoja ili inaweza kutokea kuwa yeye akapona na kusamehewa na Allah swt kwa baraka za huyo mcha Mungu.

Huyo Mcha Mungu hakuwa Aalim (aliye elimika) hivyo alipojikuta yupo pamoja na faasiqi huyo alianza kujivunia.Kwa hakika huyo mcha mungu alifikia daraja la juu sana katika ibada hali kwamba kila

kulipokucha kulimwijia kipande cha wingu likimkinga na jua na kumpatia ubaridi.Huyo Mfasiqi alipoyaona hayo yote alijiwa na hamuya laiti naye angalikuwa mcha mungu kama huyu basi naye angaliweza kufaidi hayo ambapo mwenyeji wake aliingiwa na majivuno mengi mno ya ibada zake.

Hali hii ya majivuno ya mcha mungu hayakumpendeza Mungu na badala yake alipendezewa na athari ya Mfasiqi.Ilipofika wakati wa kuagana kwaheri, huyo Mfasiqi aliondoka kwenda zake, na kumbe kile kipande cha wingu likaanza kumkinga yeye badala ya kumkinga mwenyeji wake mcha Mungu. Kwa kuyaona hayo, yalimshutusha mno huyo mcha Mungu na kujutia juu ya kosa lake asilolijua.

Basi Mtume wa zama hizo aliletewa ufunuo wa kumwambia kuwa Allah swt amemwondoshea hivyo kwa sababu ya majivuno na *istikbari* yake huyo mcha Mungu."

Basi haitupasi sisi kujivuna na kufa katika hali ya takaburi kwani aliyetukuka ni yule ambaye anayetukuzwa na Allah swt.Isije tukayapata yale tuliyoyasoma.

44. Aya Ya Qurani Zizungumziazo Tawba

Sura na Aya zifuatazo zinazungumzia *TAWBA* Qurani: (Kwanza inatangulia nambari ya sura na kufuatiwa kwa nambari ya Aya).

2:37; 2:54; 2:187; 5:71; 6:54; 9:118; 20:83; 20:122; 25:70; 25:71; 28:67; 58:13; 73:20; 4:16; 2:160; 3:89; 4:146; 5:34; 7:153; 9:5; 9:11; 16:119; 24:5; 40:7; 4:18; 7:143; 46:15; 2:279; 9:3; 2:160; 22:4; 49:11; 3:128; 4:17; 4:26; 4:27; 5:39; 9:15; 9:27; 9:106; 9:102; 25:71; 33:24; 33:73; 9:74; 9:118; 85:10; 4:17; 5:74; 9:126; 2:128; 2:54; 11:3; 11:52; 11:61; 11:90; 24:31; 66:8; 40:3; 4:17; 4:18; 4:92; 9:104; 42:25; 66:8; 3:90; 66:5; 9:112; 2:27; 2:54; 2:160; 9:104; 9:118; 24:10; 49:12; 4:16; 4:64; 110:3; 2:222; 13:30; 25:71.

45. Sifa Za Wamchao Allah

Ifuatayo ni Hotuba Na. 193 ya Imam Ali ibn Abu Talib a.s. kutoka **Nahjul Balagha**. (Sharh ya al- Hadid, Vol. 10, uk. 132-162)

Imeripotiwa na Sahaba wake Amir al- Muuminiin Ali ibn Abi Talib a.s. aliyekuwa akiitwa Hammam ibn Shurayh ambaye alikuwa mcha Mungu sana. Alimwambia Imam Ali a.s. "Ewe Amir al-Muuminiin, nielezee sifa za Muttaqiin (Wacha Mungu) kwa hali ambayo kama kwamba ninawaona wao." Imam Ali a.s. alijaribu kusita katika kumjibu na alimwambia, "Ewe Hammam, mwogope Allah swt na utende

matendo mema kwa sababu Allah swt anasema katika sura ana-Nahl Aya 128: "Kwa hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wale wanaomcha, na wale wafanyao wema."

Hammam hakuridhika kwa hayo na alimfanya Imam Ali a.s. aseme zaidi. Kwa hayo Amir al-Muuminiin a.s. alianza kwa kumtaja na kumhimidi Allah swt na kumsalia mtume Muhammad s.a.w.w. na hapo alisema:

"Amma baad, Allah swt aliyetukuka, aliyeumba viumbe. Yeye aliviumba bila ya kuwa na mahitajio ya utiifu wao au kusalimika kwao kwa utendaji wa madhambi yao, kwa sababu dhambi afanyalo mtu yeyote haimdhuru yeye na wanaomtii wala haitamfaidia kitu chochote. Yeye amewagawia miongoni mwao riziki zao na amewaweka katika nafasi zao humu duniani.

Hivyo wanaomwogopa Allah swt, hao ni watu wapambanuao, mazungumzo yao yapo mahasusi (bila ya kuongezea au kubabaisha huku na huko) na mavazi yao ni ya heshima na mwendo wao ni wenye haya (nyenyekevu). Wao huwa wanafumba macho yao kwa yale yaliyoharamishwa na Allah swt kwa ajili yao, hutega masikio yao kwa elimu ambayo inamfaidia yeye. Wao huwa daima katika hali ya majaribio (hujitaabisha kwa ajili ya dini) hata kama wao huwa katika hali ya kustarehe. Iwapo kusingekuwa kumepangiwa wakati maalum wa kufariki, basi roho zao zisingekuwa zimebakia katika miili yao hata kwa kufumba na kufumbua macho kwa sababu ya hamu yao ya kutaka malipo yao (jazaa) na kwa khofu ya adhabu za Allah swt zenye kutisha mno.

Ukuu wa Muumba upo moyoni mwao na kwa hivyo, kila kitu kilichobakia huwa ni dogo machoni mwao. Kwao Jannat (peponi au Paradiso) ni kama kwamba wanaiona na kustareheka kwa neema zake. Kwao, Jahannam (motoni au Helo) ni kama kwamba wanaiona wapo wanataabika kwa adhabu zake.

Nyoyo zao zimejaa masikitiko, wamehifadhika na maovu, miili yao ni miembamba, mahitajio yao ni machache, na nyoyo zao zipo safi. Wao wamevumilia shida kwa kitambo kidogo na badala yake wamejipatia starehe za muda mrefu. Hiyo ni biashara iliyorahisishwa na Mola kwa ajili yao. Dunia inawatamani wao, lakini wao hawaitamani kamwe. Dunia iliwateka, lakini wao walijifanya huru kwa malipo. (nafasi zao)

Amma wakati wa usiku wamekuwa wakisimama kwa miguu yao wakisoma sehemu ya Qurani na usomaji wao huwa sahihi kimizania, wakifanyia majuto na masikitiko na kuomba kwa hiyo Qurani, matibabu ya magonjwa yao. Wanapopitia Aya juu ya Shauku (ya peponi) wao huichukua kwa pupa, na nyoyo zao huzigeukia kwa shauku, nao huhisi kama kwamba hivyo vipo mbele ya macho yao.

Nao wanapopitia aya zenye khofu (za Jahannam) wao huzizingatia kwa moyo na kuhisi kama sauti za Jahannam na milio yake yanaingia masikioni mwao. Migongo yao hukunjika, husujudu juu ya vipaji vyao, viganja, magoti na vidole vyake vya miguuni na huomba kwa Allah swt ukovu wao, wakati wa mchana wao huvumilia, wakiwaona waja wa kwelikweli ambao wanamwogopa Allah swt kwa wingi. Iwapo mtu yeyote akiwatazama, watawadhania kuwa wao ni wagonjwa, ambapo wao si wagojwa kama vile wanavyodhaniwa na vile vile husemwa kuwa wamerukwa na akili. Kwa hakika, khofu ya ziada

zimewafanya wawe wendawazimu.

Wao hawaridhishwi na matendo yao yaliyo mema kwa uchache, na wala hawachukulii matendo yao makubwa kama ni makubwa. Wao huwa daima wakijilaumu na kuogopea matendo yao. Anapotokea mmoja wao akizungumzwa saidi, yeye husema: 'Mimi ninajielewa vyema kuliko vile wanielewavyo wengine, na Ewe Mola wangu! wanijua zaidi kuliko hata nafsi yangu. Ewe Allah! usinitendee kwa mujibu wa yale wayasemayo, na unifanyie mema zaidi kuliko vile wanifikiriavyo na unisamehe (zile kasoro) wao wasizozijua.'`

Alama yake ya kipekee ni kuwa utamwona yu mwenye nguvu katika Dini, mshupavu na mpole kwa pamoja, imani pamoja na kusadiki, juhudi katika (kutafuta) elimu kwa subira, ukiasi katika utajiri, upendo katika ibada, mwenye kushukuru katika njaa, mstahimilivu na mvumilivu katika hali ngumu, mapenzi katika kutafuta halali, raha katika mwongozo na chuki kwa uroho. Yeye huwa daima akitenda matendo mema lakini bado huwa mwenye woga. Ifikapo jioni huwa na shauku kubwa ya kumshukuru Allah swt. Huupitisha usiku katika khofu na huamka asubuhi katika furaha–khofu ya labda kuupitisha usiku katika hali ya usahaulifu, na furaha kwa neema na baraka alizotunukiwa na Allah swt. Ikiwa nafsi yake itakataa kustahimili kila kisichokipenda, basi naye hataikubalia ombi lake, kila kinachopendwa na nafsi yake. Macho yake yamepowa kwa yale yatakayodumu milele, ambapo vitu vya humu duniani visivyo vya kudumu, yeye hujiweka mbali navyo. Yeye huimarisha elimu pamoja na subira, na maneno yake kwa matendo.

Wewe utayaona matamanio yake ni mepesi, kasoro zake kidogo, moyo wenye khofu, nafasi iliyotosheka, chakula chake ni kidogo na cha kawaida, Dini yake ipo salama, matamanio yake yamekufa na ghadhabu yake imezimwa. Mema tu ndiyo yanayotegemewa kutoka kwake. Hapatakuwa na khofu ya kufikiwa nauovu kutoka kwake. Yeye atakuwa akihesabiwa miongoni mwa wale wanaomkumbuka Allah swt hata kama atakutwa miongoni mwa wale wanaosahau kumkumbuka Allah swt, na anapokuwa miongoni mwa wenye kumkumbuka Allah swt, hawezi kuhesabiwa miongoni mwa wenye kumsahau Allah swt. Yeye huwesamehe wale wote wasio waadilifu kwake, na humpatia yule aliyekuwa amemnyima. Yeye huwa na tabia njema hata kwa yule asiye na tabia njema mbele yake.

Kamwe hazungumzi mazungumzo yaliyo maovu, lugha yake ni laini, maovu yake hayo tena, mema yake yapo daima mbele na mizaha imeshamwondokea kwa kumgeuzia uso. Hutukuzwa pasi na kuhangaika katika maafa, mwenye subira wakati wa dhiki, na mwenye shukuru wakati wa faraja.Yeye huwa hamchukii yule anayembughudhi, na wala hatendi madhambi kwa ajili ya yule ampendaye. Yeye anakubalia yaliyo ya haki hata kabla hajatolewa ushahidi dhidi yake.Yeye hatumii kwa ubadhilifu kile kilicho mkononi mwake, wala hasahau kile atakiwacho kukikumbuka.Yeye kamwe huwa hawaiti watu kwa majina mengine yaliyo mabaya, wala huwa hawadhuru majirani zake, na wala huwa hafurahii maafa yawapatayo watu wengine, yeye kamwe hajiingizi katika ubatilifu na wala hatoki nje ya haki.

Anapokuwa kimya, ukimya wake huwa haumsikitishi na anapocheka, hapaazi sauti yake na anapotendewa mabaya, basi yeye huketi kimya akivumilia, hadi Allah swt hulipiza kisasi kwa niaba

yeke.Nafsi yake inudhika naye, na watu wamesalimika naye kwa upole wake.Yeye anajitaabisha kwa ajili ya maisha ya ahera (ya milele), na huwafikishia raha watu kutokana naye.Kujiweka kwake mbali na watu ni kwa ajili ya uchaki na kujitakasisha, na ukaribu wake kwao ni kwa ajili ya upole na rehema. Kujiweka kwake mbali si kwa ajili ya upuuzi au kujiona mwenye fahari au takabari, na ukaribu wake kwao si kwa ajili ya kuhadaa au kudanganya."

Imeripotiwa kuwa Hammam ibn Shuray alipoyasikia hayo, alizimia na kufariki papo hapo kwa kuathirika na hotuba hiyo.

Hapo Imam Ali a.s. alisema: "Kwa kiapo cha Allah swt! Hayo ndiyo niliyokuwa nikiyakhofia kwake."

Aliongezea kusema: "Mawaidha kama haya ndiyo yanavyoathiri hadi akili nzuri."

Abdullah ibn al-Kawwa (mpinzani mkuu wa Imam Ali a.s.) alisema: "Ewe Amir al-Muminiin! Je, vipi wewe hauathiriki hivyo?"

Imam Ali a.s. alimjibu: "Ole wako! Ama mauti inayo saa maalumu iliyowekewa na wala haiwezi kuzidi au kuweza kubadilishiwa. Chunga sana,usitamke tena maneno kama hayo ambayo shetani ameyaweka juu ya ulimi wako."

46. Dua Ya Imam Zaynul Aabediin Katika Kuomba Tawba

Ewe Mola wangu, ambaye sifa za kukusifu za wenye kukusifu haziwezi kutajika. Ewe mwenye mategemeo ambaye mategemeo hayawezi kwenda zaidi yako.Ewe ambaye kwako wewe malipo ya waja wako hayatapotea. Ewe unayeogopwa na waja wako. Ewe uliye khofu ya mja wako na hii ndiyo nafasi imemkuba ghafla kwa madhambi.

Ambaye amevutwa na zama za makosa na ambayo yameghalibiwa na sheitani.

Kwa hivyo ameshindwa kabisa kutimiza yale uliyokuwa umemwamrisha kuyafanya na yeye hakuyafanya.

Yeye amegang'ania tu katika yale uliyokuwa umeyaharamisha na kuyakataza kama kwamba haelewi uwezo ulionao juu yake.

Au kama yule anayekanusha ukarimu wako mtukufu kwake yeye hadi macho ya hidaya kufunguliwa kwa ajili yake na mawingu (kiza) cha upofu (wa hidaya) ulipoondolewa kutoka kwake, na alipotambua kwa

ukamilifu vile alivyojidhulumu nafsi yake na kuyazingatia kuwa amemwasi Muumba wake.

Kwa hivyo ameyaona maovu yake kwa mapana vile yalivyokuwa, akaona ukubwa na uasi na upinzani wake ulivyo kupita kiasi, kwa hivyo amekurejea wewe kwa kutaraji msaada wako kwa kuona aibu mbele yako, akielekea kwako wewe kwa hali halisi kutokana na woga wake, shauku yake ya kutaka kuondolewa kila kitu na hofu zake, ila ni wewe tu ndiye mwenye uwezo wa kuyadonoa hivyo.

Hivyo amesimama mbele yako, akiomba.

Macho yake yakiwa yanatazama chini ardhini kwa utiifu, na kichwa chake chini kwa unyenyekevu wa Ukuu wako.

Katika hali ya kudhalilika ya nafsi anaungama kwako kwa siri zake zote ambazo wewe wazijua zaidi kuliko mimi mwenyewe na katika aibu amezihisabu madhambi yake ambayo wewe umeishakwisha kumhesabia.

(Yeye anakuomba wewe kumwokoa kwa kumtoa kutoka madhambi makubwa ambayo ameingia humo wakati wewe unajua na ambavyo imemwaibisha kabisa katika heshima yako ya maamrisho yasiyotimizwa naye, starehe ambazo madhambi yamemgeukia na kumhukumia adhabu ambayo itakayokuwa daima juu yake.

Yeye kamwe hakanushi uadilifu wako, Ewe Mola wangu! Iwapo wewe utamwadhibu.

Yeye anasadiki kuwa usamehevu kwako wewe ni jambo dogo. Iwap utamsamehe na kumhurumia yeye kwani wewe ni Bwana wa Hisani, ambaye hadhanii kuwa ni vigumu kwako wewe kumsamehe madhambi hata yakiwa makubwa kiasi gani.

Ewe Mola wangu! Kwa hivyo shuhudia! Mimi nipo hapa.

Nimekuijia wewe katika Ibada (kuomba), katika hali ya utiifu wa amri zako, nikitaraji utimizo wa Ahadi yako, ambamo wewe umeahidi kujibu. Kwani wewe umesema "Niombeni, nitakuitikieni" (40:26).

Ewe Mola wangu! Mbarikie Mtume Muhammad s.a.w.w. na Ahli Bayt yake toharifu.

Naomba unijaalie msamaha wako kama vile nilivyokuijia kwa kuungama na kukiri.

Naomba uniondoe kutoka vikwazo vya madhambi kwani nimeiwasilisha nafsi yangu mbele yako. Naomba unisitiri kwa usitiri wako kama vile ulivyoweza kuuchelewesha matimizo ya kisasi chako juu yangu.

Ewe Mola wangu! Naomba unithibitishie maazimio yangu ya kukutii wewe!

Unijaalie nguvu za fahamu zangu katika kukuabudu wewe.

Nijaalie rehema ya matendo ambayo yataweza kuosha na kutoa maambukizo ya makosa niliyo nayo mimi.

Naombanife katika Dini yako na katika Ummah wa Mtume Muhammad s.a.w.w.

Ewe Mola wangu! Mimi nafanya *Tawba* mbele yako katika hali hii ya madhambi yangu yaliyo makubwa mno.

Na yaliyo madogo.
Ya makosa yangu yaliyo dhahiri na yaliyofichika na yaliyotangulia kutendwa na ambazo zimetendwa hivi karibuni kwa *Tawba* ambayo yeye hata hawezi kuisimulia nafsi yake, kwa kutotii, na wala hawezi kudhamiria kurudia maasi.

Ewe Mola wangu! Kwa hakika wewe umesema katka kitabu chako (i.e. Quran) KItukufu kuwa unazikubali *Tawba* za waja wako, na unasamehe madhambi na unawapenda wale wafanyao *Tawba* (Qurani, 1:222), naomba ukubalie *Tawba* yangu kama vile wewe ulivyoahidi. Nisamehe madhambi yangu kama vile ulivyodhamini. Nijaalie mapenzi yako kama vile ulivyokubali. Ewe Mola wangu! Nakutolea ahadi yangu kuwa kamwe *sitarudia* katika kila kile ukichukiacho; na ni dhamana yangu kuwa kamwe sitarejea katika yale usiyoyataka; na ni maahadiano yangu kuwa nitayaacha matendo yote yale yenye kukuasi wewe.

Ewe Mola wangu! Kwa hakika wewe watambua na kujua vyema kabisa kila nilichokitenda. Kwa hivyo, naomba unisamehe yale unayoyajua. Kwa uwezo wako unirejeshe kwa kile ukipendacho mno.

Ewe Mola wangu! Mimi nipo chini ya ushurutisho nisioukumbuka na baadhi ambayo nimeshakwisha sahau, lakini vyote hivyo vipo wazi mbele ya macho yako ambayo kamwe hayawezi kulala na mbele ya Ilm yako ambayo kamwe haisahau. Kwa hivyo naomba ufidie yanayostahiki kutoka kwangu. Ondoa mzigo wa yale (faradhi) juu yangu. Yafanye wepesi uzito wao kwa ajili yangu. Nihifadhi kwa kutorejelea tena karibu na hayo.

Ewe Mola wangu! Kwa hakika mimi siwezi kuwa mwanifu katika*Tawba* yangu isipokuwa msaada wako wa kunihifadhi.

Wala siwezi kujizuia na madhambi isipokuwa kwa uwezo wako.

Kwa hivyo, naomba uniimarishe mimi kwa nguvu ya kutosha na naomba unilinde kwa uhifadhi wako unaotakiwa.

Ewe Mola wangu! Kiumbe chochote kile kinapofanya *Tawba* yako na ambaye, katika ukimu yako iliyofichika, ni lazima atakiuka viapo vyake vya *Tawba* na atarejea katika madhambi na maovu yake, kwa hivyo nahitaji hifadhi yako dhidi ya kutokea kwa hayo.

Hivyo, ifanye *Tawba* yangu iwe ni majuto ambavyo stakuwa na haja ya kutubu tena – *Tawba* ambayo

tafuta yale niliyokuwa nimeyatenda na usalama kwa yale yaliyosalia.

Ewe Mola wangu! Najitetea (kutaka radhi yako) mbele yako kwa ujahili wangu.

Naomba msamaha wako kwa matendo yangu maovu.

Kwa hivyo, naomba uniingize katika hifadhi zako.

Nifunike kwa funiko zako za usalama na hisani zako.

Natubia kwako kwa kila kitu ambacho kinapingana na Amri yako au ambacho kimepoteza mapenzi yako kwa kutokana na mafikirio ya moyo wangu, maono ya macho yangu na matamshi ya ulimi wangu kwa *Tawba* ambavyo kila kiungo cha mwili wangu kisalimike kutokana na adhabu zako na kuponea kwa khofu ya maumivu ya ghadhabu zako kwa mwenye kuasi.

Kwa hivyo, nihurumie, Ewe Mola wangu, kwa unyenyekevu wangu mbele yako.

Juu ya roho yangu ambayo inadunda midundo ya kishindo kwa sababu ya khofu yako na

Juu ya maungo ya mwili wangu ambayo yanatetemeka kwa hofu yako, kwa hakika, Ewe Mwenye kutunuku riziqi, madhambi yangu yameniweka mbele yako katika hali ya kudhalilika, ili kwamba nitakapobakia kimya, basi hakuna mwingine atakaye sema badala yangu.

Iwapo nitajiombea uteteo, kwani mimi ni mtu nisiyestahiki hivyo.

Ewe Mola wangu! Bariki Mtume Muhammad s.a.w.w.na ahali Bayt yake a.s., rehema zako zinitetee maovu yangu. Yageuze maovu yangu kwa msamaha wako. Usinilipe adhabu yako kwa yale maovu yangu.

Unitandazie juu yangu kwa uarimu wako.

Nifunike kwa pazia yako.

Unitendee yale ambayo bwana mwema amfanyiavyo mambo ya huruma kwa mtumwa wake asiye na uthamini, ambaye anaomba huruma yake au mtu tajiri anapomsaidia mbele yake kiumbe chenye mahitajio.

Ewe Mola wangu! Hapana mwingine wa kunsitiri isipokuwa wewe tu, kwa hivyo Utukufu wako lazima unihifadhi. Hapana mwingine yeyote wa kunitetea kwako wewe. Kwa hivyo, huruma yako lazima inisuhulishie mimi. Kwa hakika makosa yangu yameniogopesha kupita kiasi, hivyo msamaha wako lazima yameniogopesha kupita kiasi, hivyo msamaha wako lazima unihakikishie hivyo. Kwa chochote kile nilchokwisha kukisema si kutokana na ujahili wa matendo yangu maovu, wala si kwa usahilifu wa kile kilichotangulia, cha tabia zangu zinazolaumiwa bali yasikilizwe na mbingu zako, na yale yaliyomo na ardhi yako na yale yaliyo juu yake, yanisikilize yale nilyokuambia wewe katika hali ya majuto na

masikitiko na kwa *Tawba* ambayo naombea usitiri, nikitegemea labda baadhi yako, kwa kupitia rehema zako, zinihurumie, kwa kutokana na hali yangu isiyo nzuri au udhaifu ule kwa ajili yangu labda naweza kupata dua yake inayostahili kukubaliwa kuliko maombi yangu au mateteo yaliyo na nguvu kuliko nijiteteavyo mimi na ambavyo inawekekana ikawa ni sababu ya kuokoka kwangu kutokana na ghadhabu zako na mafanikio ya ushindi wa idhini yako.

Ewe Mola wangu! Iwapo majuto na masikitiko yanatosheleza kwa *Tawba* mbele yako, basi mimi ni mjutaji sana baina ya wale wanaojuta na kusikitika. Iwap kuacha kutokutii wewe ni uongofu basi ni mwachaji mkubwa miongoni mwao. Iwapo kukuomba msamaha kunaondoa madhambi, basi mimi ni miongoni mwa wale wanaokuomba msamaha wako!
Ewe Mola wangu! Kama vile *Tawba*, umedhamiria kuzikubalia, umetutia moyo wa kusali na umetuahidi kujibu; hivyo wabariki Mtume Muhammad s.a.w.w. na kizazi chake a.s.
Nikubalie *Tawba* yangu.
Usinirejeshe nyuma kwa kutopatiwa niliyoyaazimia kutoka rehema zako.
Kwa hakika wewe ni Mkuu wa mkubaliaji wa *Tawba* za wenye madhambi na mhurumiaji kwa wenye kupotoka ambao wanarejea kwako.
Ewe Mola! Wabariki Mtume Muhammad s.a.w.w. na kizazi chake toharifu a.s. kama vile ulivyotuamrisha sisi.
Wabariki Muhammad s.a.w.w. na kizazi chake a.s. kwa baraka ambazo zitatutetea kwako siku "ya kufufuliwa na siku ya Mahitajio."
Kwa hakika wewe tu ndiye ulie na uwezo juu ya kila kitu na kila kitu ni saheli kwako wewe."

47. Mwongozo Wa Dua Zizungumziazo Tawba Katika Sahifai Sajjadiyyah

1:21–23; 9:1–2; 11:3; 12:5,7,10,12; 15:2,4; 16:33; 31:16–10; 31:14–16; 31:19–20; 31:22; 31:26; 32:15; 32:19,20; 34:3–4; 37:14; 38:3; 39:13; 40:5; 43:6; 45:9–11; 45:45; 45:52; 45:54;46:16; 47:69; 47:72–73; 47:76; 47:103; 47:86; 47:126; 48:7; 49:15,50; 51:8; 52:7;52:9;53:4.

Source URL: https://www.al-islam.org/sw/tawba-sayyid-abdul-husayn-dastghaib-shirazi#comment-0

Links
[1] https://www.al-islam.org/sw/person/sayyid-abdul-husayn-dastghaib-shirazi
[2] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/45953

[3] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/45953

[4] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/45953

[5] https://www.al-islam.org/sw/person/amiraly-m-h-datoo

[6] https://www.al-islam.org/sw/tags/tawbah